
epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Jumatano Oktoba 16, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MIAKA 30 Nipashe
Mwanga wa Jamii
www.ippmedia.com
ISSN 0856 • Na. 0581831
nipasheTZ
www.ippmedia.com
The Nipashe Digital
nipasheTZ
nipashedigital
MWANGA WA JAMII



UKURASA WA 22

## MENDY AIDAI MANCHESTER CITY BILIONI 390

**MANCHESTER,** England

BEKI wa zamani wa Manchester City, Benjamin Mendy amesema alikopeshwa fedha na wachezaji wenzake, Raheem Sterling...

## Bei ya korosho iliyononona yawatoa machozi wakulima

UKURASA 5



# Yaliyojificha mlipuko wa mauaji nchini

• **Dodoma** yaongoza, wadau walia na kasi ya ukatili huo kwa wanawake... *Endelea ukurasa 2*



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule



Dk. Hellen Kijo Bisimba



Mkurugenzi LHRC, Dk. Anna Henga

**2,438**

*Ni idadi ya wanawake waliouawa katika kipindi cha miaka mitano ikiwa ni sawa na wastani wa wanawake 492 kila mwaka au wastani wa wanawake 53 wanaouawa kila mwezi.*

UKURASA WA 3

UCHAGUZI MITAA:
**CHADEMA YALIA WANAFUNZI NAO WANAANDIKISHWA, WAZIRI AJIBU HOJA**



UKURASA WA 4

MAZUNGUMZO MAALUMU-2
KAMANDA MSSIKA
**MKASA ULIOMPATA TUHUMA ANATAKA KUNUNUA CHEO IGP**

UKURASA WA 5

**WAKILI ALALAMA KESI YA 'AFANDE' KUENDELEA BILA MHUSIKA KUWAPO**

# Sababu mbili zapaisha nauli za boti D'Salaam - Zanzibar

UK.2

**MICHEZO** CHAN KUATHIRI RATIBA YA LIGI KUU BARA UK.24

KATUNI UK.6



Wakazi wa Majohe jijini Dar es Salaam, wakipita kwenye daraja lililojengwa kwa nguvu za wananchi jana, baada ya lililokuwapo kusombwa na maji ya mvua. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Yaliyojificha mlipuko wa mauaji

**Na Grace Mwakalinga**

SIKU 33 kuanzia Septemba 1 hadi Oktoba 3, mwaka huu, kumekuwapo na mauaji kadhaa ambayo yalitokana na wivu wa mapenzi, imani za kishirikina na visasi.

Katika kipindi hicho, watu 16 waliripotiwa kuuawa katika katika mikoa ya Dodoma, Tanga, Arusha, Mara, Mwanza na Dar es Salaam, hivyo kuonesha kuongezeka kwa vitendo vya ukatili.

Nipashe imefanya tathmini ya matukio kwa kipindi hicho yakihusisha visa vya watoto sita, wanawake watano na wanaume watano kuuawa kwa kuchomwa, kuchinjwa na wengine mazingira ya kutatanisha.

Katika mkoa wa Dodoma, mauaji ya kutisha yalihusisha watoto watatu wenye umri kati ya miaka 12 na 16 akiwamo Milcah Robert (12), mhitimu wa darasa la saba katika Shule ya Msingi Chilohoni.

Wengine ni Makiwa Abdalah (16) na Salma Ramadhan (13) ambao walichomwa moto baada ya kuuawa. Pia wamo Mwamvita Mwakibasi (33) na Fatuma Mohamed (20), walipoteza maisha kwa vitendo vya ukatili, wakichomwa moto baada ya kuuawa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, George Katabazi, alitaja vyanzo vya mauaji hayo kuwa ni visasi, imani za ushirikina, na wivu wa mapenzi. Alisema kutokana na mauaji hayo, watu wanane walikamatwa na wengine watatu walifikishwa mahakamani.

### WATANO TANGA

Mkoani Tanga, watu watatu walikutwa wamechomwa moto katika msitu wa Hifadhi ya Korogwe Fuel. Watu hao ni Jonais Shao (46), mwanawe Dedan Shao (8) na Salha Hassan (18) na waliuawa baada ya kuvamiwa na watu wasiojulikana.

Mchungaji Jesse Shao, mwanafamilia wa Jonais, alisema walivamiwa nyumbani kwao na kisha walikamatwa na kupelekwa msituni ambako walichomwa moto.

Pia Saumu Ngome (19), mkazi wa kijiji cha Perani, aliuawa kikatili na mumewe, Sarah Nzuga, kwa kukatwa kichwa kwa kisu, Kamanda Mchunguzi alithibitisha kuwa chanzo cha mauaji haya ni wivu wa kimapenzi.

### WAWILI WAUAWA ARUSHA

Katika Jiji la Arusha, Johnson Josephat (39), mfanyabiashara wa vyuma chakavu, alifariki dunia akipatiwa matibabu Hospitali ya Rufani ya Mount Meru. Mke wa marehemu, Nasra Bakari, alisema mwanawe alishuhudia baba yake akipigwa na watu wanaodhaniwa kuwa ni maofisa wa polisi.

Pia David Mollel, mfanyabiashara wa madini ya ujenzi, alikutwa akiwa amening'inia kwenye mti. Mwili wa Mollel uligundulika ukiwa umening'inizwa juu ya mti kwa kutumia mkanda wa suruali huku uso wake ukifunikwa na kitambaa chekundu jirani na Mlima Oldonyowas.

Rausa Mohamed (36) mkazi wa Nyamhongolo, Mwanza, aliuawa na mume wake, Dervinus Nkabatina (46), kwa kumsukuma na kuanguka kwenye sakafu kisha kuchomwa na kitu chenye ncha kali shingoni.

Aidha, Phares Buberwa, mwanafunzi wa shule ya msingi mkoani Mara, aliuawa na mwalimu wake, Adrian Tinchwa, kwa tuhuma za kuiba simu.

### KIONGOZI WA CHADEMA

Kifo cha Ally Kibao, aliyekuwa mjumbe wa Sekretariati ya CHADEMA, mwili wake ulipatikana eneo la Ununio, Dar es Salaam, Jeshi la Polisi kupitia msemaji wake, David Misime, liliahidi kufanya uchunguzi wa kina kubaini waliohusika na mauaji hayo.

### MAONI YA WANAHARAKATI

Kutokana na mauaji hayo, mashirika mbalimbali ya haki za binadamu nchini, yameelezea wasiwasi kuhusu ongezeko la mauaji hayo. Ripoti ya Kituo cha Sheria na Haki za Binaadamu (LHRC) ya mwaka 2023, inayoonesha wastani wa wanawake wanaouawa kila mwezi imeongezeka hadi kufikia 53 kutoka 43 kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita.

Ripoti hiyo iliyozinduliwa mjini Arusha pia imeonesha kuwa mauaji mengi ya wanawake yanafanywa na ndugu wa karibu kutokana na imani za kishirikina na wivu wa kimapenzi.

Utafiti wa ripoti hiyo uliofanyika katika mikoa ya Geita, Shinyanga, Mwanza, Dar es Salaam na Kilimanjaro, pamoja na mambo mengine, ulikuwa na lengo la kutathmini kwa ujumla matokeo ya visa hivyo.

Ofisa Mwandamizi wa Masuala ya Jinsia, Wanawake, Watoto na Watu wenye Ulemavu wa LHRC, Getrude Abene, pamoja na kusisitiza kuwapo sheria zinazolinda wanawake, anaomba ushirikiano kutoka kwa mashirika yote yanayotetea haki za wanawake.

Taarifa inaonesha kuwa hadi Septemba, 2022 wanawake 2,438 wameuawa ikiwa ni sawa na wastani wa wanawake 492 kila mwaka na wastani wa wanawake 53 wanaouawa kila mwezi.

Jumuiya mbalimbali za kimataifa zimepitisha sheria za kupinga vitendo hivyo, azimio la Vienna la kupinga mauaji ya wanawake na wasichana, pamoja na azimio la kimataifa la Baraza la Haki za Binadamu linazitaka nchi wanachama Tanzania ikiwamo, kufanya juhudi za kutokomeza mauaji ya wanawake.

Mwanaharakati wa haki za wanawake nchini, Judith Singibara, anasema katika kutokomeza mauaji dhidi ya wanawake, kuna haja ya kuwashirikisha wanaume katika kampeni za kupinga ukatili wa kijinsia.

"Mapambano ya kuwalinda wanawake na aina zote za unyanyasaji yamekuwa yakisikika, wanaharakati wa haki za wanawake wanasema bado kuna maeneo mengi yanahitaji kurekebishwa, ili kumlinda mwanamke na kuna haja ya kuwashirikisha wanaume na wavulana katika kampeni za kupinga ukatili," anasema.

Kwa mujibu wa Ripoti ya Jeshi la Polisi inayohusu Makosa ya Jinai dhidi ya binadamu mwaka 2022 watu 2,464 waliuawa na mwaka 2023 ilikuwa ni 2,303 sawa na asilimia 6.5 ya visa hivyo.

Naye Mwanaharakati wa Haki za Binadamu, Dk. Hellen Kijo-Bisimba, anasema: "Ni dhahiri kwamba kuna ongezeko la mauaji nchini na ni muhimu serikali kuchukua hatua za haraka ili kulinda haki za raia. Tunahitaji kuwa na mfumo wa sheria unaotekelezeka ili kuzuia vitendo vya ukatili na kuhamasisha jamii kutoa taarifa kwa polisi."

## Sababu mbili zapaisha nauli za boti Dar-Z'bar

**Na Waandishi Wetu**

NAULI za usafiri wa majini Dar es Salaam-Zanzibar zimepanda. Wananchi wanalalama ugumu wa maisha umeongezeka.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar, Mtumwa Said amesema kuongezeka kwa bei ya mafuta ya meli kumesababisha kupanda kwa bei ya nauli ya boti kutoka Sh. 30,000 ya awali hadi Sh. 35,000 sawa na ongezeko la Sh. 5,000 (asilimia 16.7).

Mtumwa alisema jana visiwani Zanzibar kuwa ongezeko hilo la bei ya mafuta limesababisha gharama za uendeshaji kuongezeka kwa asilimia 21.

Mkurugenzi Mtumwa alisema kupanda kwa bei ya dola sokoni kumechangia ongezeko la nauli kwa kuwa kampuni za usafirishaji majini (boti) zinapolipa kodi, kununua vifaa na kufanya matengenezo ya vyombo vyao, hulipa kwa dola.

Alisema kuwa mwaka 2022, dola ya Marekani iliuzwa kwa wastani wa Sh. 2,330, lakini mwaka huu, inauzwa kwa wastani wa Sh. 2,850 katika soko la kawaida, hivyo kufanya kuwapo ongezeko la gharama za uendeshaji.

Mkurugenzi huyo alisema serikali imeridhia kampuni za uwekezaji zinazotoa huduma za usafiri wa baharini kuongeza bei za nauli za usafiri kati ya Dar es Salaam na Unguja kwa daraja la chini kutoka Sh. 30,000 hadi 35,000. Nauli mpya zilianza kutumika rasmi Oktoba 7, mwaka huu.

Alifafanua kuwa nauli ya Sh. 30,000 kwa daraja la chini ilitangazwa mwaka 2022, kipindi ambacho bei ya mafuta ilikuwa Sh. 2,500 kwa lita kulinganishwa na mwaka huu ambapo bei ya mafuta ni Sh. 3,020. Sababu nyingine, Mtumwa alisema ni gharama za matengenezo na utawala, kampuni zikilalamika kuongezeka gharama za utawala na matengenezo ya vyombo kipindi hiki ambacho dola imepanda.

"Bei iliyopendekezwa awali ilikuwa zaidi ya Sh. 35,000 iliyokubaliwa. Serikali kwa kuzingatia hali za maisha ya wananchi wake, hasa wa daraja la chini, katika mazungumzo yaliyofanyika, tuliwaomba sana wawekezaji, kampuni hizi kukubali ombi la serikali kufikia Sh. 35,000 kwa daraja la chini na kampuni zilitukubalia," alisema.

Mtumwa aliwataka wadau wote wa usafirishaji baharini kuzingatia bei iliyoidhinishwa na serikali. Atakayekiuka, atachukuliwa hatua kali za kisheria.

Hata hivyo, nauli ya boti kutoka Unguja kwenda Pemba haijapanda, imeendelea kuwa Sh. 20,000 kwa daraja la chini.

Baadhi ya wananchi waliozungumza na Nipashe jana, walisema nauli mpya zitaongeza ukali wa maisha, wakiomba serikali kuangalia uwezekano wa kuweka ruzuku ili kuwasaidia wananchi wa kipato duni. Said Ali Abdalla, Salma Juma Khalfan na Rahma Abadalla Mussa, wakiwa eneo la kukata tiketi za boti, jijini Dar es Saalam jana, walisema wamesikitishwa na ongezeko hilo la nauli kwa kuwa wananchi wengi hali zao ni duni.

**Imeandikwa na Rahma Suleiman (ZANZIBAR) na Halfani Chusi (DAR)**

## HABARI KITAIFA

UCHAGUZI MITAA:

# CHADEMA yalia wanafunzi kuandikishwa, waziri ajibu

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimetaja kasoro 18 mbalimbali zilizoko kwenye uandikishaji wa wapigakura kwenye Daftari la Wakazi ulioanza Oktoba 11, mwaka huu.

Awali, Oktoba 13, mwaka huu, Katibu Mkuu wa ACT Wazalendo, Ado Shaibu, alitaja kasoro tano ambazo zimetajwa pia na CHADEMA ikiwamo kuandikishwa kwa watoto ambao hawajatimiza miaka 18.

Wakati malalamiko hayo yakitolewa, jana Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, alijibu hoja hizo kwamba kila Mtanzania mwenye umri wa miaka 18 anaandikishwa bila kujali ni mwanafunzi au la.

Mkurugenzi wa Itifaki, Mawasiliano na Mambo ya Nje wa CHADEMA, John Mrema, alizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam na kutaja kasoro 18 ambazo wamezibaini katika uandikishaji.

Alitaja kasoro ya kwanza kuwa vituo vya uandikishwaji kuwekwa kwenye majengo au nyumbani kwa viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), akisema jambo hilo limetokea katika maeneo mbalimbali kama Korin Kusini, Kitongoji cha Rau Jimbo la Moshi Vijijini.

Kasoro ya pili ni waandikishaji kuruka namba kwenye madaftari ya kuandikisha wapigakura, wakiamini kuwa lengo la kufanya hivyo ni baadaye kuja kuingiza majina feki. Alitaja kasoro ya tatu kuwa ni kuandikishwa kwa wanafunzi ambao hawajafikisha miaka 18 na kuendelea.

Mrema alitaja kasoro ya nne kuwa ni baadhi ya waandikishaji kuwa wanachama wa CCM na tano ni wenyeviti wa mitaa, vijiji na vitongoji ambao wako madarakani kuwa sehemu ya mawakala.

Kasoro ya sita ni viongozi na wanachama wa CCM kupeleka majina ya waandikishwaji.

Alitaja jambo la saba kuwa ni vituo vya uandikishwaji kuwekwa kwenye kambi ya vyombo vya ulinzi na usalama, nane ni uandikishaji kuanza kabla ya muda uliowekwa kwa mujibu wa kanuni za uchaguzi na tisa ni baadhi ya wakuu wa wilaya kuingilia shughuli ya uandikishaji.

Jambo la 10, kwa mujibu wa Mrema, ni waandikishaji kuacha vituo na kwenda kuandikisha mitaani na kasoro ya 11 ni mawakala wa CHADEMA kutoruhusiwa kuingia kwenye vituo vya uandikishaji. Pia alisema kuna uandikishaji wa majina hewa na waandikishaji kuongeza majina ya watu ambao hawakufika kwenye kituo na pia mawakala kuzuiwa kuondoka na idadi ya watu walioandikishwa.

Jambo la 15, alisema ni watu kuandikishwa nje ya kituo na 16 ni kukamatwa kwa wanachama na viongozi wa CHADEMA na Jeshi la Polisi.

Mwenyekiti wa CHADEMA Mkoa wa Songwe, Isakwisa Lupembe, alisema katika Jimbo la Tunduma, watoto wanachukuliwa shuleni kwenda kuandikishwa, hoja iliyopingwa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Tunduma, Mariam Chaurembo, ambaye ni msimamizi wa uchaguzi katika jimbo hilo.

Waziri Mchengerwa, akizungumza na waandishi wa habari jijini Mwanza, alisema pamoja na mambo mengine, wizara hiyo imehakikisha inatoa elimu kwanza kuondoa mkanganyiko wa wananchi kuchanganya kati ya uandikishwaji katika Daftari la Kudumu la Mpigakura na Daftari la Wakazi la Serikali za Mitaa.

"Tukiri kuwa suala hili bado linahitaji kutolewa elimu kwani mchakato wa uchaguzi ni wa mwaka mzima na haufanywi tu kwenye wizara hiyo bali ni wa kila Mtanzania aliyefikisha umri wa miaka 18 pamoja na vyama vyote vya kisiasa," alisema.

Pia alisema jukumu hilo linavihusu pia vyama vya kisiasa, hivyo si vyema kulalamika kuwa elimu haijapelekwa bali na wao wanatakiwa kuhakikisha wanatoa elimu kwa wanachama wao.

Alisema elimu inaendelea kutolewa kupitia wakuu wa mikoa, wilaya, vyombo vya habari pamoja na wakurugenzi katika halmashauri kupitia hamasa na ufafanuzi wa hoja mbalimbali zinazoibuka pamoja na taasisi zaidi ya 83 zilizoomba kutoa elimu hiyo katika maeneo yote nchini.

"Tumesikia kuwa kuna uandikishwaji wa watoto ambao hawajakidhi vigezo bado hatujapata uthibitisho wa masuala hayo lakini nitoe maelekezo kwa wasimamizi na wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi kuhakikisha wanafuata sheria, taratibu na kanuni zilizotolewa," alisema Mchengerwa.

Kuhusu wasimamizi wa vituo kukataa kutoa takwimu, alisema suala hilo lipo kwa mujibu wa sheria za uchaguzi na kuwa jukumu lao ni kuhakikisha wanaandika kila mwananchi mwenye vigezo huku mawakala wakiwa na jukumu la kuwatambua waliokwenda kujiandikisha ili kujua kama ni halali.

Alisema baada ya hatua hiyo, kitakachofuata ni kuwaorodhesha wote waliojiandikisha na kubandika katika maeneo husika, ili kubaini kasoro na kuzifanyiwa marekebisho.

Waziri alisema kanuni hizo zimeandaliwa na kupitishwa kwa ushirikiano na vyama vyote 19, hivyo viongozi wa vyama wanatakiwa kutambua ni namna gani ya kushughulika na mazingira wanayobaini kuwa yana kasoro.

Kuhusu vituo bandia, alisema hakuna suala kama hilo na kuwa vituo vyote vinavyotumika vipo kisheria ambavyo ni 80,812 kati ya mitaa, vijiji na vitongoji 68,543.

Alisema pamoja na mambo mengine ipo mikoa iliyofanya vyema kwa kipindi hicho cha siku nne kwa kuvuka asilimia 54.2 ikiwa ni pamoja na Mkoa wa Tanga, Ruvuma, Njombe, Songwe, Lindi na Iringa.

Kadhalika alitaja mikoa ambayo bado ipo nyuma kuwa ni pamoja na Katavi, Kilimanjaro, Geita, Kigoma na Manyara huku mikoa yenye watu wengi ambayo bado iko chini ya asilimia 40 kama zilivyoainishwa kwenye mabano Dar es Salaam (35.3), Mwanza (34.2), Morogoro (37.9), Dodoma (38.5), Tabora (27.7) na Kagera (34.8).

***Imeandikwa na Vitus Audax (MWANZA), Jenipher Gilla (DAR) na Moses Ng'wat (TUNDUMA)***

**Kwa maoni: +255 677 020 701**
**Email: customerrelations@guardian.co.tz**


## DAR RAPID TRANSIT AGENCY

DART
DAR RAPID TRANSIT

## Request for Expression of Interest to Invest in Transit-Oriented Development (TOD) at Gerezani BRT Terminal in Dar es Salaam.

The **Dar Rapid Transit (DART) Agency** is a governmental entity established by **Government Notice (GN) No. 120 of 25th May 2007 under the Executive Agencies Act No. 30 of 1997.** The Agency's mandate is to **plan, develop, and manage an efficient public transport system** in Dar es Salaam to reduce traffic congestion, promote sustainability, and improve urban mobility.

1. The Agency owns a parcel of land in a prime area located at Gerezani, Ilala District in Dar es Salaam, measuring approximately a total of 19,000m2, which is planned for accommodating **TRANSIT-ORIENTED DEVELOPMENT(TOD). The area is divided into two lots:**
   a) Lot One: 8,000 square meters
   b) Lot Two: 11,000 square meters
2. Developers may express interest in developing either one or both lots. Each lot must be submitted separately but under the same conditions and address.
3. The objective is to transform the Gerezani BRT Terminal into a more appealing customer-oriented hub to complement the transport services with them, but not limited to: -
   **i. Supermarkets**
   **ii. Retail Shops/Stores**
   **iii. Malls**
   **iv. Residential and**
   **v. Small Traders (Machinga)**
   **vi. Parkings**
4. To foster BRT services, the Agency plans to develop the referred piece of land under a Joint Venture model in a form to be agreed upon by both parties (investors).
   Therefore, the Agency seeks an eligible, reputable, competent investor(s) who powerfully demonstrates the appropriate muscles, experience, and expertise in designing and investing in the referred TOD at Gerezani BRT Terminal.
5. The developer may express interest in a Joint Venture (JV), but the JV must still meet all legal and technical requirements, with defined roles and responsibilities for each member.
6. This advert serves to invite sealed submission of the Expression of Interest from eligible and reputable investors to formally express their interest in investing in the referred TOD at Gerezani BRT Terminal under the Joint Venture or Design, Build, Finance, Operate/Maintain and Transfer **(DBFOMT)** Arrangements.
7. Those who are interested and find themselves to be eligible for investing in the referred TOD MUST avail the Agency with the following paper qualifications: -
   i. Expression of Interest letter
   ii. Company Profile
   iii. Document establishing the company (certified copies)
   iv. Pre-proposal design
   v. Feasibility study/business plan
   vi. Proposed financing model
   vii. Cost estimates
   viii. Audited Financial Statement for the past three (3) years
   ix. Profit-Sharing Proposal
   x. Proof of experience investing in a similar large-scale project for at least **Seven (7) years** worth at least **Tsh 100 billion.**
8. Expression of Interest MUST be accompanied by a proof of availability of funds for the proposed TOD project in either form from the reputable financing institution(s)
9. **NOTE:** This is not an invitation to tender
10. Interested investors who may wish to visit the area for the proposed TOD are humbly encouraged to do so and should contact the responsible Officer via Mobile No. +255 784632208 effectively from 16th October, 2024 to 30th October 2024.
11. A request for clarification MUST be in writing and reach the office of the undersigned at the latest five (5) days before the deadline for submission of the expression of interest.
12. The Agency has the mandate to accept or reject any submission and, if necessary, may annul the entire expression of interest process at any time without consideration for the interested investors.
13. Expression of interest in a sealed envelope marked **"EXPRESSION OF INTEREST FOR TRANSIT ORIENTED DEVELOPMENT (TOD) AT GEREZANI BRT TERMINAL** must be submitted on or before 30th October 2024 and should be either physically or electronically delivered to the address below:

**Chief Executive**
**Dar Rapid Transit Agency,**
**Ubungo Maji, Morogoro Road,**
**P.O. Box 724,**
**DAR ES SALAAM, Tanzania.**
**Email: ce@dart.go.tz**

## KAMANDA MSSIKA

# Mkasa alipotuhumiwa anataka kununua u-IGP

Na Romana Mallya

***Jana katika ufafanuzi wake alipozungumza na Nipashe, Kamanda mstaafu Abdallah Mssika alieleza safari ya maisha yake, akianzia kwenye ufundi gereji hadi kushika nafasi mbalimbali ndani ya Jeshi la Polisi, ikiwamo kuwa Msaidizi wa Inspekta Jenerali wa Polisi (IGP). Endelea...***




Kamanda Abdallah Mssika akiwa katika ofisi za gazeti Nipashe, Mikocheni, Dar es Salaam.

KAMANDA Mssika anasimulia matukio binafsi ambayo hawezi kuyasahau maishani mwake kwa miaka 40 aliyotumikia Jeshi la Polisi kuwa ni pamoja kutuhumiwa kutaka kununua ateuliwe kushika nafasi ya IGP mwezi Januari 2006.

Anaeleza kwa kina matukio manne akikumbuka pia, shambulio la bomu katika Ubalozi wa Marekani nchini.

"Nikiwa Kamanda wa Polisi Shinyanga, matapeli kutoka Dar es Salaam waliwasiliana na mimi kwa njia ya simu kwa kunipongeza kuwa ni miongoni mwa baadhi ya makamanda waliomo katika orodha ya kuteuliwa na Rais Jakaya Kikwete katika nafasi ya IGP kwa vile IGP aliyekuwapo kwa wakati ule alikuwa anastaafu," anasimulia.

Kamanda Mssika anasema mwakilishi wa matapeli hao aliyekuwa anawasiliana naye, alimjulisha kwamba wao ndio walikuwa katika kamati maalum ya kuteua na kwamba kati ya makamanda waliokuwamo katika orodha ya mwisho, yeye (Mssika) alikuwa anaongoza kwa sifa za juu.

"Hakuishia hapo, akaniambia kwa vile kamati yao imetakiwa kuwasilisha jina langu kwa Mheshimiwa Rais mara tu atakapomaliza kuzungumza na baraza lake la mawaziri aliokwishawateua na mhasibu wa Ikulu yuko pamoja katika msafara wa Mheshimiwa Rais, hivyo, akanitaka nitume fedha za kujikimu haraka ili wakamilishe kazi yangu.

"Nilitambua mara moja ni matapeli, nikikumbuka tukio la matapeli kutaka kumtapeli Mkuu wa Wilaya ya Lindi (wakati huo) Fatuma Mikidadi, nikiwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi mwaka 2003," anasimulia.

Kamanda Mssika anasema kuwa katika tukio la mkuu wa wilaya huyo, walimlaghai na kumtisha kwamba alikuwa ni mmoja wa wakuu wa wilaya waliokuwa katika orodha ya wenye sifa ya kuteuliwa na Rais Benjamin Mkapa kuwa wakuu wa mikoa.

"Walimtisha kuwa kinachomwangusha ni 'kiongozi aliyejilimbikizia mali isivyo halali' na kamati yao iliyoundwa kumshauri Rais watapendekeza afukuzwe kazi na kukabidhiwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kwa hatua zaidi.

"Wakamtaka awatumie haraka Sh. milioni tatu kwa njia ya huduma ya Posta Western Union, huduma ambayo hata hivyo wakati huo ilikuwa haijafika Lindi. Walikamatwa wote," anasimulia.

Kutokana na tukio hilo, Kamanda Mssika anasema alipopigiwa simu kwamba yumo katika orodha ya wanaopendekezwa kwa nafasi ya IGP, alibaini haraka "hizo ni mbinu za matapeli" kutokana na uzoefu wake kazini.

"Yaani kamanda nitoe fedha kuhonga wasaidizi wa Rais na Amir Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama ili niteuliwe kuwa IGP!" Kamanda Mssika anamtaka kwa msisitizo na hisia.

Anasema kitendo cha watu kujiamini mpaka kufikia kujenga ujasiri wa kuwafuata makamanda kadhaa wa polisi, yeye akiwa ni miongoni mwao ili kuwatapeli, aliona ni uhalifu mkubwa na wana uwezo wa kufanya chochote, ikiwa ni pamoja na udhalilishaji taasisi nyeti kama Jeshi la Polisi.

"Nikiwa Shinyanga, matapeli waliowasiliana na mimi, nikawaaminisha wanachofanya ni sahihi, lengo waamini kwamba wamenipata na kuwaaminisha wanachofanya ni sahihi na msaada wao utakuwa na faida kwangu.

"Ndipo nilipowasiliana na Ofisi ya Mkuu wa Upelelezi Kanda ya Dar es Salaam (ZCO) na kumweleza picha kamili na hatua nilizochukua kuhakikisha wanakamatwa Dar es Salaam waliko.

Kamanda Mssika anasema walikubaliana makachero wawapo uwanja wa ndege ili atakapotua wawakamate kwa mbinu waliyokubaliana. Anasema kuwa baada ya kutua na kutoka nje ya uwanja wa ndege, upande wa abiria wanaowasili, awali hakuona mtu yeyote akimfuata; si matapeli wala kachero.

Anasema kuwa baadaye wakati anaangaza macho huku na huko, alimwona kachero mwandamizi (bila kumtaja jina) aliyekuwa anaongoza timu ya makachero katika ukamataji huo ambaye alimweleza kwamba tayari wameshawakamata matapeli hao.

"Akaniambia 'Afande Mssika, pole kwa safari, wale matapeli tumeshawakamata'. Nilihoji mmewakamataje? Akanijibu 'hapana, mazingira ya mipango ya awali yalibadilika baada ya matapeli wale kuonekana wakiwa airport (uwanja wa ndege)'.

"Hivyo, ofisa kiongozi wa timu ya ukamataji akanifafanulia kwamba, 'tulivyowaona tu afande, tuliwatambua mara moja kuwa ndio timu yenyewe ya utapeli wa aina hiyo', tukajua bila shaka kwamba ndio wenyewe'.

"Akaniambia wamekamatwa watuhumiwa wanne na tayari walikuwa wamepelekwa Kituo Kikuu cha Polisi Dar kwa mahojiano na uchunguzi zaidi, lakini washirika wenzao wengine walitoroka kabla hawajakamatwa," anasimulia.

Kamanda Mssika anasema wakati wa harakati za kuwakamata matapeli hao, alikuwa amehamishwa kutoka Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga kwenda kuwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha na amri ilikuwa imeshatolewa.

"Wakati nikisubiri asubuhi kukuche ili niende kwa ZCO na baadaye Makao Makuu ya Polisi, asubuhi magazeti yakawa yameandika 'RPC atapeliwa kwa ahadi ya kuwa IGP, aliambiwa mipango imeiva naye akaingia, akatoa Sh. milioni 2.5'.

"Sijakwenda kwa ZCO wala kuandika maelezo yangu, tayari mambo yamekwenda mbali. Hata kwenda Makao Makuu ya Polisi kumwona IGP kumweleza niko safarini kuelekea Arusha, safari haikuwapo kwa sababu uhamisho ukawa umefutwa siku hiyo hiyo.

"Ninachofikiria mpaka sasa na ndicho ninachoamini, kilichofuata baada ya hapo ni mimi badala ya kwenda Arusha nikapelekwa kuwa Mkuu wa Utawala na Fedha Kanda Maalum ya Dar es Salaam nikiwa chini ya Kamishna Alfred Tibaigana baada ya (kitengo hicho) kuundwa kwa mara ya kwanza na Rais Kikwete," anasimulia.

Kamanda Mssika anasema hakukaa muda katika kitengo hicho, akapelekwa kuwa Kamanda Polisi Mkoa wa Kagera kuchukua nafasi ya Kamanda (Venance) Tossi aliyehamishiwa Makao Makuu kwa kazi nyingine na baadaye akateuliwa kuwa Msemaji wa Jeshi la Polisi nchini.

"Kamanda mwenye tamaa ya kuwa IGP kwa kuhonga, inawezekanaje huyo huyo kupewa majukumu hayo kuanzisha Kanda Maalum Dar es Salaam, Tibaigana akiwa hayupo anakaimu majukumu hayo na kwenda Kagera kuwa kamanda na hatimaye kuwakilisha Jeshi la Polisi kama msemaji?" anahoji.

Kamanda Mssika anasema taasisi mbalimbali zilizomhoji na kwa maelezo aliyotoa, yalionekana na mamlaka za kiuchunguzi ndio sahihi kuliko yale ya awali yaliyosambazwa na vyombo vya habari.

"Sikupata mrejesho kama maelezo yangu ndio sahihi isipokuwa kwa vitendo kwa kuwajibika kupewa nafasi mpaka hatimaye kustaafu, nikatunukiwa medali nyingine na nishani ya utumishi uliotukuka.

"Mpaka sasa sifahamu waliofanya hivyo ni nani, zaidi ya waliokamatwa. Siwezi kujua ni nani? Namna gani au wapi ilifanyika? Lakini hatimaye nilikuja kuaminika," anasema.

Mbali na medali na nishani Kamanda Mssika aliaminika hadi kuwa mwalimu wa Chuo cha Polisi Kurasini (Dar es Salaam) kuanzia mwaka 1990-1996, akifundisha makachero masomo ya Upepelezi wa Makosa ya Jinai, yakijumuishwa pia matukio ya makosa ya wizi wa kalamu/kughushi.

"Ualimu ambao mafunzo yangu ya kuwa CID nilipata Uingereza katika Chuo cha Detective Training School kilichoko mji wa Wakefield, West Yorkshire England kwa ufadhili wa British Council. Tulikuwa na wenzangu 10 na ilikuwa mwaka 1990.

"Lengo la mafunzo haya ni baada ya serikali kupanga kujenga chuo kikuu cha makachero kimataifa CID Ukanda wa Kusini mwa Afrika ambacho kingekuwa Dodoma.

"Baada ya mafunzo, nikapelekwa Chuo cha Polisi Kurasini kufundisha walimu wa walimu ambao ni timu ya awali. Nilikaa chuoni miaka sita na baadaye kupelekwa Makao Makuu ya Jeshi la Polisi kuwa Msaidizi Aid de Camp (ADC) wa IGP Omar Mahita.

### AJALI YA HELIKOPTA

"Tukio lingine ninalokumbuka ni ajali ya helikopta iliyotokea Nachingwea, tukiwa na IGP akizunguka kukagua maeneo yale. Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi alifariki dunia. Hili ni tukio la kukumbuka," anasema.

### SHAMBULIZI UBALOZINI

Kamanda Mssika anasimulia tukio lingine ambalo hatosahau ni baada ya kutolewa kwa IGP na kupelekwa Kituo cha Polisi Oysterbay kuwa OCD.

Katika utekelezaji majukumu hayo mapya, anasema kulitokea shambulizi la bomu katika Ubalozi wa Marekani nchini.

"Dakika 20 au 30 wakati tukio linatokea siku hiyo ilikuwa ni paredi ya OCD ambapo huwa na mkusanyiko wa askari wengi. Wakati linatokea tulikuwa tumemaliza ukaguzi wa paredi, askari wanaingia katika magari kwenda doria.

"Awali tulidhani mlipuko huo ulitokea bandarini, lakini kupitia askari waliokuwa pointi ya Kenyatta wakati huo, walitujulisha kupitia radio call kuwa ni ubalozini.

"Tulitoka moja kwa moja kwenda eneo la tukio, tukadhibiti eneo vizuri. Msaada tuliotoa uliwezesha vielelezo muhimu kupatikana kwa haraka," anasema.

Kamanda Mssika anataja matukio mengine yaliyokuwa yanatokea wakati huo ni migomo ya wanafunzi wa chuo kikuu ambayo walikuwa wanayashughulikia kwa utaratibu anaotaja "mzuri ambao ulifanikisha kurejesha utulivu".

***ITAENDELEA KESHO**

HABARI KITAIFA

## Wakulima wafurahia kupanda bei ya korosho

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

WAKULIMA wa korosho Wilaya ya Masasi, Mtwara na Nanyumbu wa Chama Kikuu cha Ushirika (MAMCU) wamejikuta wakibubujika na machozi ya furaha baada ya kuuza korosho zaidi ya tani 18, 000 kwa bei ya juu ya Sh. 4,195 na bei ya chini Sh. 3,440.

Mnada wa kwanza wa korosho msimu wa 2024/2025 wa chama hicho uliofanyika katika kijiji cha Nakachindu, Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, tani zaidi ya 18,000 za korosho ziliuzwa kwa njia ya mfumo wa soko la bidhaa (TMX).

Wakizungumza katika mnada huo baadhi ya wakulima walisema kuwa bei hizo hazijawahi kutokea katika misimu ya hivi karibuni kwenye zao la korosho.

Feith Milanzi, mkulima wa kijiji cha Nakachindu alisema kuwa bei ya Sh. 4,195 kwa bei ya juu na Sh.3,440 bei ya chini zinaleta matarajio makubwa katika maisha yao.

Alisema matunda hayo ya bei nzuri katika mazao ya biashara hasa korosho yanatokana na uongozi bora wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

Naye Faraja Hassani, mkulima kutoka wilaya ya Nanyumbu alisema takribani miaka saba hadi kumi iliyopita bei ya zao la korosho ilikuwa chini na kuwakatisha tamaa.

"Tunampongeza Rais Samia Suluhu kwa kusikiliza kilio chetu wakulima cha kutaka bei za mazao hasa korosho kuwa bora kwa wakulima na leo tunaona bei zimekuwa juu sana na kila mkulima ameridhika," alisema.

Mkurugenzi wa Bodi ya Korosho Tanzania, Francis Alfred, alisema bei za mazao zitaendelea kuwa nzuri na wakulima watafaidika.

# Mkuu wa chuo kikaangoni kwenye Baraza la Maadili

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

BARAZA la Maadili leo linatarajia kufanya kikao cha uchunguzi wa kina kuhusu malalamiko ya ukiukwaji wa maadili yanayomkabili Mkuu wa Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA), Prof. Eliamini Sedoyeka.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Kamishna wa Maadili, Jaji Mstaafu Sivangilwa Mwangesi, baraza hilo lina jukumu hilo kwa mujibu wa kanuni ya 11 ya Kanuni za Maadili ya Viongozi wa Umma za mwaka 2017.

Jaji Mwangesi alibainisha kuwa uchunguzi huo utakuwa wa wazi na utafanyika leo na kesho jijini hapa kwa mujibu wa kifungu cha 25(5) na 29(6) cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Sura 398.

"Kikao hicho cha uchunguzi kitafanyika Oktoba 16 hadi 17 mwaka huu, jijini Dodoma," alisema.

Awali alibainisha kuwa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ina jukumu la kuchunguza tabia na mwenendo wa kiongozi wa umma yeyote kwa madhumuni ya kuhakikisha masharti ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma yanazingatiwa.

"Hivyo, sekretarieti imepeleka malalamiko kwenye Baraza la Maadili kuhusu tuhuma za ukiukwaji wa maadili kwa viongozi hawa wa umma wawili," alisema.

Alisema sekretarieti hiyo ni taasisi inayojitegemea chini ya Ofisi ya Rais iliyoanzishwa kwa mujibu wa Ibara ya 132 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 kutekeleza Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Na. 13 ya Mwaka 1995.



Wahitimu wa darasa la saba na baadhi ya walimu wa Shule ya Msingi Blue Tanzanite, Kata ya Endiamtu, mji mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, wakicheza muziki wakati wa mahafali yao, shuleni hapo juzi.
**PICHA: GIFT THADEY**

## Wakili alalama kesi ya 'afande' kuendelea bila mhusika kuwapo

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Dodoma leo inatarajiwa kuanza kusikiliza shauri linalomkabili Fatma Kigondo, maarufu Afande, anayeshtakiwa kwa madai ya kuwatuma vijana kumbaka kwa kundi na kumwingilia kinyume cha maumbile binti mkazi wa Yombo Dovya, Dar es Saalam.

Kogondo anakabiliwa na shtaka la kubaka kwa kundi kinyume cha kifungu cha sheria namba 131 A kifungu kidogo cha pili ambacho kinasema anayewasaidia wahalifu kutenda kosa la ubakaji na yeye anahusika kwenye ubakaji wa kundi.

Hakimu Mkazi Mwandamizi, Nyamburi Tungaraja, alisema mahakamani hapo jana kuwa shauri hilo litaanza kusikilizwa leo bila kujali kama mshtakiwa atakuwapo au la.

"Shauri hili litaanza kusikilizwa kesho (leo) bila kujali kama mshtakiwa atakuwapo au hatakuwapo. Kwa hiyo tukutane kesho saa 3:00 asubuhi," alisema Hakimu Tungaraja.

Kuhusu maombi ya wakili wa mlalamikaji, Peter Madeleka, ya kukamatwa na kuwekwa rumande mshtakiwa kwa sababu za usalama wake, Tungaraja alisema hawezi kutoa amri ya kumkamata mtu kwa kushindwa kufika mahakamani mara moja.

"Siwezi kutoa amri ya kukamatwa kwa mshatakiwa kwa kushindwa kuja mara moja mahakamani. Lakini pia ugonjwa ni sababu ambayo ipo kisheria, hivyo kesi hii itaendelea tu hata kama hatakuwapo ama atakuwapo kesho (leo) mahakamani lakini pia dhamana ni haki ya mshtakiwa," alisema.

Akizungumza na waandishi wa habari nje ya mahakama, Wakili Madeleka alisema hawakubaliani na mwenendo wa shauri hilo linavyoendeshwa na hakimu huyo na wanajiandaa kulihamishia mahakama kuu.

"Mshtakiwa siku ya kwanza hakuja na leo (jana) pia hajafika lakini leo (jana) ilikuwa siku ambayo mahakama hii inakwenda kutoa uamuzi kuhusu maombi yangu mawili, likiwamo la kukamatwa na kuwekwa rumande kwa mshtakiwa kwa sababu za kiusalama kama ilivyo kuwa kwa watuhumiwa wengine kina Nyundo na wenzake. Pia ombi la pili lilikuwa mahakama kutoa adhabu kwa mshtakiwa ya kukiuka amri ya mahakama na kushindwa kufika wakati wa shauri.

"Lakini tunashangaa leo hii hakimu anasema yeye hawezi kutoa amri ya mahakama kukamatwa na kuwekwa rumande kwa mtuhumiwa huyo kwa madai kuwa dhamana ni haki ya mshtakiwa kwani wale kina Nyundo walikuwa hawana haki ya dhamana. Tunafahamu kuwa makosa kama haya ya ulawiti mahakama huwa inaondoa dhamana kwa washtakiwa na kuwaweka rumande kwa sababu za kiusalama," alisisitiza Madeleka.

Shauri hilo ambalo lilipangwa kusikilizwa Oktoba 7, 2024 liliahirishwa hadi jana baada ya mshtakiwa kutofika mahakamani kwa madai kuwa ni mgonjwa. Siku hiyo Wakili Madeleka aliomba mahakama kutoa amri ya kukamatwa kwa Kigondo na kumwekwa rumande katika Gereza la Isanga jijini hapa.

Wakili Madeleka alisema anaiomba mahakama hiyo kutoa amri hiyo ili mshtakiwa huyo akamatwe mara moja na kunyimwa dhamana kama ilivyokuwa kwa washtakiwa wengine.

"Mheshimiwa hakimu tunaomba mahakama yako tukufu itoe amri ya mshtakiwa kukamatwa na kuwekwa rumande na kuondolewa dhamana kwa sababu ya usalama wake kama ambavyo mahakama imekuwa ikitoa amri hizi kwa washtakiwa wengine.

"Lakini pia kutokana na mshtakiwa kutofika mahakamani hapa amevunja amri ya mahakama ambayo inamtaka kufika kila tarehe ya shauri lake, hivyo tunaomba mahakama itoe adhabu kali mara moja kwa mshtakiwa kuvunja amri ya mahakama ya kumtaka kufika kila shauri linapoendeshwa kwani kukosekana kwake hapa leo kesi hii haiwezi kuendelea," alisema Madeleka.

"Kama anaumwa lazima wangeleta ushahidi wa daktari kama ambavyo wanatakiwa kufanya kwa mujibu wa sheria lakini hii kusema tuu mtu anaumwa siyo kazi ya mahakama kubaini kama mtu anaumwa kweli au haumwi walipaswa kuleta ushahidi wa kimatibabu hapa siyo kuzungumza tu," alihoji wakili Madeleka.

Hakimu Tungaraja aliahirisha shauri hilo hadi leo na hoja hizo zinatarajiwa kutolewa uamuzi.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wananchi watumie muda uliowekwa kujiandikisha uchaguzi Serikali za Mitaa

**KAZI** ya kujiandikisha kwa ajili ya uchaguzi wa serikali za mitaa inaendelea sehemu mbalimbali nchini. Wakati hilo likiendelea, viongozi wakuu kitaifa wamekuwa wakiwahimiza wananchi kushiriki mchakato huo ili kuwa na sifa za kuwachagua viongozi wanaofaa.

Viongozi hao si tu wanafanya hivyo kinadharia bali kwa vitendo kwa sababu wameshuhudiwa wakijiandikisha katika maeneo yao ili nao washiriki kuwachagua watu watakaosimamia shughuli za maendeleo na kuwaongoza wananchi kutatua changamoto zilizoko kwenye sehemu husika.

Katika kufanya hivyo, wakati wa kufunguliwa kwa pazia la kujiandikisha, Rais Samia Suluhu Hassan alifanya hivyo Chamwino mkoani Dodoma huku Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango akijiandikisha nyumbani kwao, Buhigwe mkoani Kigoma. Mbali na Rais na makamu wake, viongozi wengine kama vile mawaziri na wakuu wa mikoa wamejiandikisha huku wakiwataka wananchi waige mfano huo.

Viongozi hao wametoa kauli mbalimbali kuelezea umuhimu wa kushiriki uchanguzi huo na kuonya kuwa asiwapo mtu yeyote wa kufanya hujuma katika mchakato mzima. Rais Samia, kwa mfano, ameonya mara kadhaa kuhusu dosari zozote zitakazojitokeza huku akitaka uchaguzi huo usilitie doa taifa.

Uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliopangwa kufanyika Novemba 27, mwaka huu, ni wa muhimu na wananchi wanapaswa kushiriki kikamilifu katika kuchagua viongozi bora watakaosukuma gurudumu la maendeleo katika maeneo husika. Viongozi na wananchi hao ndio wanaojua kwa undani matatizo yanayowakabili, hivyo kuchagua viongozi bora ni hatua mojawapo ya kuyatatua.

Kwa mantiki hiyo, jambo la muhimu ni wananchi kujiandikisha na kufanya mchakato katika kura za kuchagua wagombea wenye sifa katika ngazi ya chama. Uchaguzi huu ndilo chimbuko rasmi la demokrasia na utawala bora, kwa hiyo ni muhimu kila mwananchi mwenye sifa za kushiriki asikose.

Kupitia serikali za mitaa, wananchi kwa kushirikiana na viongozi wao, wana uwezo wa kuainisha kero zinazowakabili na kutafuta mbinu za kuzishughulikia pamoja na kujiletea maendeleo endelevu.


Kero kama vile maji, barabara, kilimo, mifugo, afya na elimu katika maeneo husika, watatuzi wa kwanza ni wananchi wenyewe. Kupita uchaguzi wa serikali za mitaa, kwa kuchagua viongozi bora ndilo suluhisho katika kutatua kero hizo.

Kama wahenga wasemavyo kwamba majuto ni mjukuu, wananchi wajitokeze kujiandikisha kwa ajili ya kushiriki uchaguzi huo muhimu kwa mustakabali wao na kinyume cha hapo watajikuta hawapigi hatua kutoka walipo sasa kwa sabau ya kutokushiriki. Kawaida, baadhi ya wananchi wamekuwa wazito katika kushiriki uchaguzi na matokeo yake wanapopatikana viongozi wabovu au wasiofaa, hujikuta wakilaumu bila kujua kosa limeanzia kwao.

Kama alivyosema Rais Samia juzi kwamba uchaguzi wa serikali za mitaa ni muhimu kwa sababu utasaidia unaonesha ushiriki wao katika masuala ya maendeleo sambamba kubuni, kupanga na kutekeleza mipango yao, Watanzania kamwe wasikose kushiriki kwenye mchakato huo kwa manufaa yao.

Ni vyema wananchi wakatumia muda uliopangwa kujitokeza kwa wingi kujiandikisha katika daftari la wakazi ili kuwa na sifa za kupiga kura. Viongozi katika mitaa na vyama vya siasa ni muhimu wakaendelea kuwahimiza wananchi kujiandikisha ili kupata nafasi ya kupiga kura siku ya uchaguzi itakapowadia.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita. 0713 578284,
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Majina ya mipaka vijiji, vitongoji ni muhimu uchaguzi huu Serikali za mitaa

**UCHAGUZI** wa serikali za mitaa unafanyika wiki ya mwisho ya mwezi ujao, ni Jumatano Novemba 27, ukihusisha vijiji 12,333, mitaa 4,269 pamoja na vitongoji 64,274.

Kabla ya kufanyika uchaguzi, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mohamed Mchengerwa anatangaza rasmi majina ya mipaka ya mitaa, vijiji na vitongoji.

Lakini uzoefu unaonyesha kuwa kumekuwapo na sintofahamu ya kutozingatia mipaka wakati wa kubandika majina ya wapigakura kwenye vituo vya kupigia kura katika maeneo mbalimbali.

Kwa mfano, katika uchaguzi wa serikali za mitaa uliopita, baadhi ya watu walikwenda katika vituo vya kupigia kura na kukuta majina yao hayapo, wakaambiwa si wa mtaa huo waliouendea, kwa sababu ya mipaka. Walipokwenda wa jirani wakaambiwa huko nako hawapo, kwamba huo si mtaa wao. Vilevile, wengine majina yao yalibandikwa kwenye vituo ambayo si vya mitaa wanayoishi.

Hivyo, wakati huu ambao serikali imetangaza mipaka, ingekuwa ni vyema suala la kubandika majina ya wapigakura nalo likazingatia mipaka hiyo ili kuwapunguzia usumbufu wananchi na kuona kama kuna figisu. Nadhani si vyema kama mtu anaishi mtaa A anafika kituoni anakosa jina lake, anaambiwa akaangalie mtaa B ambako nako halipo au hata kama lipo, atachagua viongozi ambao si wa mtaa wake na hakuwaazimia tangu mwanzo.

Kwa hiyo ingekuwa ni vyema TAMISEMI ikahakikisha kero kama hiyo haitokei tena katika uchaguzi unaokuja ili kila mwenye sifa za kupigakura aweze kushiriki katika uchaguzi huo bila kikwazo.

Sintofahamu hiyo imo ndani ya uwezo wa ofisi hiyo hivyo, ijitahidi kuchapisha majina ya wapigakura kulingana na mipaka ya sasa, ili kila mmoja atambue eneo atakalokwenda kupigakura. Vinginevyo, yanaweza kujirudia yale ambayo yamewahi kujitokeza katika uchaguzi uliopita na kusababisha baadhi ya watu kukata tamaa baada ya kuhangika huku na kule kutafuta majina yao kwenye vituo.

**Rais huyo wa kwanza wa Tanzania, kwa kutumia falsafa yake hiyo ya kilimo, aliwaagiza viongozi wa serikali na wananchi kushiriki, shabaha yake kuu ikiwa ni kuinua uchumi wa vijijini na kuboresha maisha ya wananchi.**

Serikali ijitahidi kuwafahamisha wananchi majina ya maeneo na mipaka itakayohusika kujiandikisha na upigaji wa kura, ili wajue maeneo yao. Kikubwa ni kuwa majina yasibandikwe vituo vingine. Lakini si vibaya wapigakura wakapewa elimu ya kutosha kuhusu mipaka ya maeneo yao kwani inawezekana wapo wasioijua ili siku ikifika wajue watakwenda kituo gani kupiga kura, lakini wakute majina yao.

Inaweza kukatisha tamaa kama mtu anaishi mtaa A halafu anakwenda kwenye kituo chake anakuta jina halipo limebandikwa kituo cha mtaa mwingine. Mtindo huo unaweza kusababisha usumbufu usio wa lazima.

Mipaka ina umuhimu wake, kwani inaondoa mkanganyiko wa kijiografia ambao unaweza kujitokeza na kusababisha wapigakura kwenda vituo vingine badala ya kule wanakoishi.

Kwa maana hiyo, wananchi kutambua mipaka ya maeneo yao ni jambo la msingi, lakini pia kubandikwa majina kwenye vituo ambavyo wanapigia kura ni jambo lingine muhimu ili wasisumbuke. Ikumbukwe kuwa kila unapofanyika uchaguzi wa serikali za mitaa, kuna kero ambayo wapigakura hukumbana nayo, ambayo ni kukosa majina yao katika vituo vya kupigia kura kutokana na mipaka mipya ya mitaa inayowekwa na serikali kila mwaka wa uchaguzi wa serikali za mitaa.

Mipaka huwekwa kulingana na jinsi mtaa unavyozidi kupanuka. Lakini tatizo huwa linajitokeza ni kukosekana kwa majina ya baadhi ya wapigakura katika vituo vyao kuchagua viongozi.

Hivyo, yale ambayo yamekuwa yakijirudia kila mwaka wa uchaguzi wa serikali za mitaa wakati wa kuweka mipaka, yangeishia mwaka 2019 ili mwaka huu kila kitu kiende sawa bila usumbufu.

## HABARI KITAIFA

# Bajeti dawa za saratani kuongezwa kila mwaka

**Na Joseph Mwendapole**

WAZIRI wa Afya, Jenista Mhagama, amesema serikali itaendelea kuongeza bajeti ya dawa za saratani kila mwaka kutokana na ongezeko kubwa la wagonjwa wa saratani.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati akizindua Kituo cha Tiba na Utafiti wa Saratani cha Shifaa Kinondoni jijini Dar es Salaam. Alisema wakati idadi ya wagonjwa ikiongezeka wagonjwa wengi wanaougua ugonjwa huo hawana uwezo wa kugharamia matibabu na wanahitaji kusaidiwa.

Alisema kwa mwaka huu wa fedha pekee serikali imetenga Sh. bilioni 10 kwa ajili ya kununua dawa za saratani na kila bajeti mpya kiasi hicho kitakuwa kikiongezeka.

Alisema kituo hicho kitaongeza upatikanaji wa huduma muhimu za kiuchunguzi na kitabibu kwa matatizo yanayohusu ugonjwa wa saratani nchini.

Alisema saratani imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka na takwimu za kila mwaka zinaonyesha kuwa na ongezeko na mwaka 2022 wagonjwa wapya wa saratani walikuwa 45,000.

"Wagonjwa wa saratani wasipowahi kupata matibabu inawasababishia vifo kwa hiyo unapokuwa na wagonjwa 45,000 nchi lazima iweke mipango ili kuokoa uhai wa wananchi hao kwa kupata tiba mapema," alisema.

Alitaja saratani zinazoongoza kuwa ni ya mlango wa kizazi (24.2%), tezi dume (10.7%), matiti (10%), koo (7.9%), utumbo mpana (4.9) ya aina zote za saratani nchini.

Waziri Mhagama alisema saratani zote hizo zinachukua asilimia 42 ya idadi ya wagonjwa wote wanaougua nchini na zinazoathiri zaidi wanawake nchini ni ya mlango wa kizazi na matiti.

"Ndiyo maana serikali imeamua kuchukua jitihada za kukinga wananchi wake dhidi ya saratani na pale ambapo mtu anapata saratani apate matibabu na leo Shifaa wanapounga mkono juhudi za serikali kuokoa wagonjwa wa saratani na kuwarejeshea furaha tunawashukuru sana," alisema Mhagama.

Alisema serikali imeendelea kutoa elimu na kufanya kampeni maalum za uchunguzi na utambuzi wa mapema wa maradhi ya saratani na kupanua huduma za uchunguzi kwenye mikoa mbalimbali nchini.

Alisema lengo ni kuhakikisha kunakuwa na vituo vingi vya utoaji wa huduma hizo na hasa kwa wanawake na serikali imeimarisha huduma za uchunguzi wa kimaabara na huduma za radiolojia kwa kuhakikisha inakuwa na mashine 85 za CT-SCAN za kutosha na MRI.



Wafanyabiashara wadogo, wakiwa wamepanga bidhaa zao chini, wakisubiri wateja katika eneo la Kariakoo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Serikali yasisitiza matumizi akili mnemba, roboti

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imesema matumizi ya akili mnemba na roboti katika sekta mbalimbali ni muhimu, kwa kuwa ina uwezo wa kuboresha huduma za kijamii na kukuza uchumi kwa njia ambazo zilikuwa hazifikiriki miaka michache iliyopita.

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Jerry Silaa, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akifungua kongamano la nane la mwaka la Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Kongamano hilo ambalo linafanyika kwa siku tano lilianza Jumapili na kushirikisha wadau mbalimbali wa TEHAMA kutoka ndani na nje ya nchi ambao wameshiriki katika utoaji mada mbalimbali zinazohusu wanawake na vijana.

Waziri Silaa alisema, matumizi ya akili mnemba na roboti katika sekta ya afya, yanaweza kusaidia kutoa utambuzi wa haraka wa magonjwa na kuboresha huduma za afya za msingi.

"Katika kilimo, zinaweza kuboresha tija kwa wakulima kwa kusaidia katika usimamizi bora wa uzalishaji na utafiti wa hali ya hewa.

"Teknolojia hizi zinaweza kubadilisha kabisa namna tunavyoendesha biashara na utengenezaji wa bidhaa, kwa kuboresha mifumo ya usambazaji na kuongeza ufanisi," alisema.

Waziri Silaa alisema kwa kutumia teknolojia hizo, viwanda vinaweza kuongeza uzalishaji na kuwa na ushindani mkubwa kwenye soko la kimataifa.

Pia, alisema zinaweza kuimarisha mifumo ya elimu kwa kusaidia upatikanaji wa elimu bora kwa kila mwanafunzi, bila kujali eneo au hali yake ya kiuchumi.

"Kwa njia hii, tunaweza kuhakikisha kuwa kila Mtanzania anapata fursa ya kujifunza na kuchangia katika maendeleo ya taifa letu.

"Nimatumaini yangu kuwa kongamano hili litawezesha kujifunza zaidi na kupata uzoefu kuhusu matumizi sahihi ya Akili Mnemba na Roboti, ili kuboresha utendaji kazi na utoaji huduma," alisema.

Alisema, Tanzania kama ilivyo kwa nchi nyingi zinazoendelea, inakabiliwa na changamoto hasa kwenye jamii ambazo zinahitaji suluhisho la haraka na endelevu.

Alisema kwa kutumia teknolojia hizo, zitasaidia kuzitatua kwa kuongeza ufanisi, kupunguza gharama na kuleta ubunifu katika sekta mbalimbali.

Kongamano hilo ni fursa ya kutafakari na kujadili hatua za kuchukua ili kuhakikisha kuwa teknolojia hizo zinatumiwa vyema kwa manufaa ya taifa bila kuathiri masuala ya kiuchumi, kiusalama na tamaduni.

Alisema anaamini baada ya kongamano, watapata taarifa inayojumuisha maono kuhusu maendeleo ya TEHAMA, pamoja na mapendekezo ya namna ya kuboresha Sera na Sheria za kisekta, ili kuchochea ukuaji na matumizi katika kuchangia Pato la Taifa na kutoa huduma kwa wananchi.

Alisisitiza serikali imeendelea kuwekeza kwa kasi kubwa katika TEHAMA ambayo ndio nguzo kuu ya kufikia uchumi wa kidijitali.

Kongamano hilo limebebwa na kaulimbiu: "Kutumia Uwezo wa Akili Mnemba na Robotiki kwa Mapinduzi ya Kiuchumi na Kijamii."

Waziri Silaa alisema kaulimbiu hiyo inafungua mjadala muhimu kwa wakati huu ambao dunia nzima inashuhudia mapinduzi ya kidijitali, na kama nchi ina nafasi ya kuzitumia kuboresha ustawi wa wananchi na kuongeza tija.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Mohammed Khamis Abdulla, alisema kesho (Alhamis) katika kongamano hilo kutatolewa tuzo za kimataifa ambazo Tanzania imekuwa nchi ya kwanza mwenyeji wa mashindano yaliyoandaliwa na Umoja wa Afrika, kuhusu masuala ya akili mnemba na roboti.

Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya TEHAMA, Dk. Nkundwe Mwasaga, alisema kongamano hilo lilitanguliwa na mkutano wa wanawake na TEHAMA pamoja na vijana na TEHAMA, ambapo masuala mbalimbali yalijadiliwa.

## KABWELA

Na Fadhil Mohammed



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

# MWITO WA KUTOA MAONI KUHUSU MAOMBI YA VIBALI VYA UJENZI NA LESENI KUTOKA EWURA

***Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ni taasisi ya udhibiti wa huduma za sekta nne mchanganyiko inayojitegemea, iliyoundwa kwa Sheria ya EWURA Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania. Shughuli kuu za Mamlaka ni pamoja na kudhibiti kiufundi na kiuchumi sekta za Nishati na Maji kwa Tanzania Bara. EWURA ina wajibu wa kudhibiti shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ndogo ya Mafuta na Gesi Asili.***

Sheria ya Mafuta Na. 21 ya mwaka 2015 inaipa nguvu EWURA, kusimamia shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli. Kifungu cha 126 (1) cha sheria hiyo kinamtaka mtu yoyote anayetaka kujenga miundombinu ya mafuta kuomba kibali cha ujenzi kutoka EWURA. Aidha, Kifungu cha 131 (1) cha sheria hiyo kinawataka wote wanaojihusisha na sekta tajwa kuwa na leseni iliyotolewa na EWURA.

EWURA imepokea maombi ya vibali vya ujenzi na leseni kutoka kwa waombaji walioorodheshwa hapa chini. Kutokana na kifungu cha 19(4) cha Sheria ya EWURA, Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania, taarifa inatolewa kwa umma kwamba, wafuatao wameomba vibali vya ujenzi ili wajenge miundombinu ya mafuta na leseni kwa ajili ya kujihusisha na biashara/shughuli katika mkondo wa kati na chini wa sekta ya mafuta ya petroli.

| S/N | Jina la Mwombaji | Eneo | Jina la Mkurugenzi/Uraia | Aina ya Ombi la Leseni/Kibali cha Ujenzi |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Front Oil Fuel Service Station, S.L.P 360, Shinyanga. | Kiwanja Na. 5, Kitalu "J", Eneo la Bwiligu, Chalinze, Pwani. | Fredy Simoni Upiro (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 2. | Maganzo (Mfs) Energy, S.L.P. 68217, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 129, Kitalu "VV", Eneo la Limele, Bagamoyo, Pwani. | Charels Pius Tungu (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 3. | Freddy Simon Upiro T/A Front Oil Fuel Service Station, S.L.P 360, Kahama. | Kiwanja Na. 5, Kitalu "G", Eneo la Msolwa, Chalinze, Pwani. | Freddy Simon Upiro (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 4. | Mek One Industries Ltd, S.L.P 5055, Dar es Salaam. | Eneo Mbezi Luis Ubungo, Dar es Salaam. | Mohamed Eidha Awadh (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 5. | Luftwafee Holdings Limited, S.L.P 1477, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 237, Kitalu "D", Eneo la Kunduchi, Kinondoni, Dar es Salaam. | Innocent Kilenga (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 6. | Oilcom (T) Ltd - Msasani CCBRT, S.L.P 20831, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 1008, Kitalu "G", Eneo la Msasani, Kinondoni, Dar es Salaam. | Ameir Munif Abdallah Nahdi (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 7. | George Filling Station, S.L.P 246, Mtwara. | Kiwanja Na. 4, Kitalu "A", Eneo la Mangaka, Nanyumbu, Mtwara. | George Raphael Binali (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 8. | Matemba Fuel Petrol Station, S.L.P 141, Morogoro. | Kiwanja Na. 12, Kitalu Na. 23, Eneo la Magubike, Kilosa, Morogoro. | Dickson Naftal Matemba (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 9. | Kigwe Filling Station, S.L.P 2993, Dodoma. | Eneo la Kigwe, Bahi, Dodoma. | Elidy S Rutuma (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 10. | Ruaha Milling Company Limited Fuel Service Station, S.L.P 2145, Iringa. | Kiwanja Na. 47, Kitalu "A", Eneo la Ndiuka, Iringa. | Athanas Paul Kipeto (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 11. | Gobsan Company Limited, S.L.P 32164, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 143, Kitalu "L" Eneo la Mpomvu, Geita. | Ibrahim Mohamed Bashe (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 12. | Richard Kasubi Mfungi, S.L.P 645, Geita. | Kiwanja Na. 4, Kitalu "K", Eneo la Mpovu, Geita. | Richard Kasubi Mfungi (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 13. | Chibole Petrol Station, S.L.P 8049, Mwanza. | Kiwanja Na. 1524, Kitalu "A", Eneo la Iwelyashinga, Ilemela, Mwanza. | Mjaya Lawi Chibole (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 14. | Renatus Chikata Pima T/A PIMAZ, S. L. P 18076, Nkwenda. | Eneo la Mabira, Kijiji cha Kakanja, Kyerwa, Kagera. | Renatus Chikata Pima (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 15. | Yuda Yakobo Bucheyeki Fuel Filling Station, S.L.P 113, Shinyanga. | Kiwanja Na. 24, Kitalu "A", Eneo la Salawe, Shinyanga. | Yuda Yakobo Bucheyeki (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 16. | Samora2020 Oil & General Supply Co. Ltd - Chunya, S. L. P 35, Chunya. | Kiwanja Na. 15, Kitalu "D", Eneo la Kibaoni, Chunya, Mbeya. | Samora Mussa Muyombe (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 17. | Tairo Oil Limited - Rujewa Petrol Station, S.L.P 222, Rujewa. | Kiwanja Na. 230, Kitalu "U", Eneo la Rujewa, Mbarali, Mbeya. | Mangera Machera Marwa (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 18. | Saatatu Investment Limited, S.L.P 14, Mbozi. | Kiwanja Na. 70 & 71, Kitalu "B", Lubele - Ibanda, Kyela, Mbeya. | Yona Saatatu Chaula (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 19. | Ndonyalo Energies - Njoomlole Petrol Station, S.L.P 59103, Njombe. | Eneo la Njoomlole, Uwemba, Njombe | Beno Paulo Ndonyalo (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 20. | Msigwa Logistic and Timber Suppliers Limited, S.L.P 497, Mafinga | Kiwanja Na.223, Kitalu "A", Jogoo, Makambako, Njombe. | Furahisha Franci Msigwa (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 21. | Afroil Investment Ltd - Kahama Petrol Station, S.L.P 38383, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 290, Kitalu "U", Eneo la Nyasubi, Kahama, Shinyanga. | Hilmi Ahmed Mbaraka (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 22. | Samo Christopher Roche Filling Station, S. L. P 872, Musoma. | Kijiji cha Mambali, Nzega, Tabora. | Samo Christopher Roche (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 23. | Africa Energy Ltd, S.L.P 22786, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 4, Kitalu "U", Eneo la Nyasubi, Kahama, Shinyanga. | Edha Nahdi (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 24. | Gapco Tanzania Limited – Meru Gapco Service Station, S.L.P 9103, Dar es Salaam. | Barabara ya Sokoine, Eneo la Posta, Arusha. | Ellon Kanyingi Kamau (Raia wa Kenya) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 25. | Total Tanzania Limited – Kibo Service Station, S.L.P 1503, Dar es salaam. | Barabara ya Mahakamani, Eneo la Philips, Arusha. | Mamadou Ngom (Raia wa Senegali) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 26. | Amlate Petrol Station, S.L.P 60, Karatu. | Shamba Na. 725/1, Kijiji cha Ngorbob - Kisongo, Arumeru, Arusha. | Agnes Joseph Mushy (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 27. | EDCO Investment, S.L.P 3175, Morogoro. | Kiwanja Na. 25, Kitalu "A", Eneo la Mji Mpya, Morogoro. | Daudi Godwin Makuri (Mtanzania) | Leseni ya Jumla ya Vilainishi (*Lubricant*) |
| 28. | Ahmed Abdallah Bakhamis T/A Happy Oil Mvomero, S.L.P 20, Kilosa. | Kiwanja Na. 1, Kitalu "A", Eneo la Kisaki, Kilosa, Morogoro. | Ahmed Abdallah Bakhamis (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 29. | Yunus Hassan Mfalla T/A Iyumbu Filling Station, S.L.P 502, Dodoma. | Kiwanja Na. 5, Kitalu "AJ", Eneo la Iyumbu, Dodoma. | Yunus Hassan Mfalla (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 30. | Admire Oil Limited, S.L.P 7494, Dodoma. | Kiwanja Na. 10, Kitalu "G", Eneo la Makulu, Dodoma. | Said Mire Artan (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 31. | Job Bosco Fuime Petrol Station, S.L.P 200, Mpwapwa. | Kiwanja Na. 61 & 62, Kitalu 'D', Eneo la Pwaga, Mpwapwa, Dodoma. | Jobu Bosco Fuime (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 32. | Olympic Petroleum(T) Ltd-Singida, S.L.P 391, Singida. | Kiwanja Na. 322 & 323, Kitalu "HH", Eneo la Mwenge, Singida. | Ally M. Adon (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 33. | Lubevo Co. Limited, S.L.P 13989, Dar es Salaam. | Eneo la Tabata, Ilala, Dar es Salaam. | Ayman Hijaz (Raia wa Uingereza) | Leseni ya Jumla ya Vilainishi (*Lubricant*) |
| 34. | Alharthy Logistic Company Ltd, S.L.P 5559, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 138 Kitalu "G", Eneo la Boko Magengeni, Kinondoni, Dar es Salaam. | Mussa Issa Abdallah (Mtanzania) | Leseni ya Jumla ya Vilainishi (*Lubricant*) |
| 35. | United Energy Limited, S.L.P 7494, Dar es Salaam. | Eneo la Mbagala Kizuiani, Temeke, Dar es Salaam. | Mohamed Said Ismail (Raia wa Kenya) | Leseni ya Jumla ya Mafuta |
| 36. | Premier Energies Limited, S.L.P 15816, Dar es Salaam. | Msasani Peninsula, 1040, Haillasie road, Kinondoni, Dar es Salaam. | Khadija A Mohamed (Mtanzania) | Leseni ya Jumla ya Mafuta |
| 37. | Skeu Investment Company Limited, S.L.P 6678, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 2048, Kitalu "E", Eneo la Ukonga, Ilala, Dar es Salaam. | Stellah Kabaka Melkiony (Mtanzania) | Leseni ya Jumla ya Mafuta |
| 38. | Suncom Oil Limited, S.L.P 104, Dar es Salaam. | PSSSF twin Tower, 31st Floor, Ilala, Dar es Salaam. | Sunday Severine Mohubuta (Mtanzania) | Leseni ya Jumla ya Mafuta |
| 39. | Lake Gas Limited, S.L.P 5055, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 46, Kitalu "E", Eneo la Vijibweni, Kigamboni, Dar es Salaam. | Stephen Mtemi (Mtanzania) | Leseni ya Jumla ya Gesi ya Kupikia (LPG) |
| 40. | Johari Rotana, S.L.P 14909, Dar es Salaam. | Eneo la Kisutu, Ilala, Dar es Salaam. | Evancs Chimwenjo (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta kwa Matumizi Binafsi |
| 41. | Stecol Corporation, S.L.P 76182, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 370, Eneo la Upanga, Ilala, Dar es Salaam. | Zeng Yun (Raia wa China) | Leseni ya Kituo cha Mafuta kwa Matumizi Binafsi |
| 42. | Harbours Asset Rental Limited, S.L.P 13412, Dar es Salaam. | Eneo la Yombo Vituka, Temeke, Dar es Salaam. | Emir Karamagi (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta kwa Matumizi Binafsi |
| 43. | Herera Supplies Limited, S.L.P 33448, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 238 Eneo la Ufipa, Kinondoni, Dar es Salaam. | Honest Anselim Temba (Mtanzania) | Leseni ya Usambazaji wa Gesi ya Kupikia (LPG) |
| 44. | Kazingawe Investment Company Limited, S.L.P 310, Dar es Salaam. | Eneo la Mtoni Kijichi, Temeke, Dar es Salaam. | John Nangawe (Mtanzania) | Leseni ya Usambazaji wa Gesi ya Kupikia (LPG) |
| 45. | Alharthy Logistics Company Limited, S.L.P 5559, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 138 Kitalu "G", Eneo la Boko Magengeni, Kinondoni, Dar es Salaam. | Mussa issa Abdallah (Mtanzania) | Leseni ya Usambazaji wa Vilainishi (*Lubricant*) |
| 46. | Offshore Partners Tanzania, S.L.P 23201, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 423, Kitalu "D", Eneo la Msasani, Kinondoni, Dar es Salaam. | Michael Kimei (Mtanzania) | Leseni ya *Condensate Dealership* |
| 47. | Top Oil Petroleum Co. (T) Ltd - DMB Petrol Station, S.L.P 42445, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 144/1, Kitalu "B", Eneo la Buyuni, Ilala, Dar es Salaam | Dahir Mbarak Salim (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 48. | Victoria Service Station Limited, S.L.P 75467, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 2096, Kitalu "E", Eneo la Boko, Kinondoni, Dar es Salaam. | Harold Elisamehe Matemba (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 49. | Victoria Service Station Limited, S.L.P 75467, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 35, Kitalu Na. 1861, Eneo la Victoria, Kinondoni, Dar es Salaam. | Harold Elisamehe Matemba (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 50. | Simba Oil Kilungule Service Station. S.L.P 40451, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. P16158, Eneo la Mbagala Kilungule, Temeke, Dar es Salaam. | Farid Salim Mbarak Nahdi (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 51. | Mansoor Industries Limited, S.L.P 80218, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 64 & 65, Eneo la Vijibweni, Kigamboni, Dar es Salaam. | Shanif Mansoor Jamal (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 52. | Vivo Energy Tanzania Limited, S.L.P 78470, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 263, Kitalu "D", Eneo la Kurasini, Temeke, Dar es Salaam. | Mohamed Bougriba (Raia wa Tunisia) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 53. | M&P Exploration Production (T) Ltd, S.L.P 80460, Dar es Salaam. | Eneo la Madimba, Mtwara. | Nicolas Engel (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta kwa Matumizi Binafsi |
| 54. | Edith Kibali Miaka Elfu Moja, S.L.P 92, Mtwara. | Eneo la Chikongola, Mtwara. | Amon Sengati (Mtwara) | Leseni ya Usambazaji wa Gesi ya Kupikia (LPG) |
| 55. | GF Vehicle Assemblers Limited S.L.P 22692, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 673, Kitalu "A", Eneo la Viwanda la TAMCO, Kibaha, Pwani. | Imran Mehboob Karmali (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta kwa Matumizi Binafsi |
| 56. | Hass Petroleum (T) Ltd - Kibaha, S.L.P 78341, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 22, Eneo la Kongowe, Kibaha, Pwani. | Abdulkadir Ahmed Hussein (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 57. | Calvary Filling Station, S.L.P 30153, Pwani. | Eneo la Boko Mnemela, Kibaha, Pwani. | Bildard Rogathe Lema (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 58. | Fountain Petroleum Limited, S.L.P 826, Mtwara. | Eneo la Mtama, Lindi. | Mehboob Osman (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 59. | Olasiti Investment Co Ltd, S. L. P 10275, Arusha. | Kiwanja Na. 2211, Kitalu "E", Eneo la Buhongwa, Nyamagana, Mwanza. | Vicent Innocent Amani (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta. |
| 60. | Ndinga Filling Station, S.L.P 36, Misungwi - Mwanza. | Kiwanja Na. 14, Kitalu "D", Eneo Misungwi, Mwanza. | Deo Mayalla (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 61. | River Oil Petroleum (T) Limited, S.L.P 10415, Mwanza. | Kiwanja Na. 12, Kitalu "A", Eneo la Bugolora, Ukerewe, Mwanza. | Gabriel Mugini Kenene (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 62. | Ashico Petrol Station, S.L.P 149, Magu. | Kiwanja Na. 11, Kitalu "T", Eneo la Isandula, Magu, Mwanza. | Arbogsti O. Shirima (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta. |
| 63. | Blue Wave Emporium Limited, S.L.P. 11624, Mwanza | Kiwanja Na. 1733, Kitalu "B", Eneo la Igombe, Ilemela, Mwanza. | Ephraim Stanley Fimbo (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 64. | Karantini Fuel Filling Station, S.L.P 497, Tarime. | Kiwanja Na. 1 Kitalu "C", Tarime Mara. | William Nchagwa Karantini (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 65. | Kiagata Filling Station, S.L.P 1418, Musoma. | Eneo la Nkyankoma, Nyamimange, Butiama, Mara. | Chacha Mashauri Chirare (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta. |
| 66. | Karagwe Oils Company Limited S.L.P 484, Karagwe. | Kiwanja Na. 21, Kitalu "A" Bukombe, Geita. | Seleman Zahoro Mansoor (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 67. | NGS Petroleum Ltd-Geita Mbugani, S. L. P 20, Simiyu. | Kiwanja Na. 1, Kitalu "S", Eneo la Mbugani, Geita. | Njalu D. Silanga (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta. |
| 68. | Nekemia Phillimon Tiigwera, S.L.P 61, Karagwe. | Kiwanja Na. 3, Kitalu "C", Eneo la Kihanga, Karagwe, Kagera. | Nekemia Phillimon Tiigwera (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |

***Mtu yeyote au kikundi cha watu wenye pingamizi kwa mwombaji yeyote aliyetajwa hapo juu kwamba asipewe leseni au Kibali cha ujenzi, anatakiwa kuwasilisha pingamizi hilo kwa EWURA ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya tangazo hili kupitia anwani tajwa hapa chini.***

**Imetolewa na**

**Mkurugenzi Mkuu,**
**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji**



# Wananchi, mifugo watumia maji ya bwawa Itilima

**Na Shaban Njia,** KISHAPU

WAKAZI wa Kijiji cha Itilima Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu mkoani Shinyanga wamedai kukumbwa na magonjwa ya kuhara na kutapika kwa kutumia maji ya bwawa kwa ajili ya kunyweshea mifugo yao.

Madai hayo yalitolewa na Consolata Msonge wakati akizungumza na Nipashe kwa niaba ya wakazi hao na kuhusu madhara wanayopata kwa kutumia maji hayo ambayo si salama kwa afya zao, licha ya kijiji chao kuwa jirani na Kijiji cha Mwagala Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga ambako kuna mradi wa majisafi na salama ya Ziwa Victoria.

Consolata, alisema wanalazimika kutembea umbali wa kilomita hadi 10 kwenda kuchota maji na kukosa muda wa kufanya shughuli zao za kiuchumi.

Alisema wakati mwingine wanalazimika kutumia maji ya kwenye bwawa hilo na kuhatarisha maisha yao kwa kushambuliwa na fisi majira ya alfajiri, wanyama ambao nao huenda kunywa maji hayo.

Esther Daniel, alisema wanadamka alfajiri kwenda kuchota maji kwenye bwawa hilo kabla hayajatibuliwa na wanyama na kurejea majumbani mchana.

Mwenyekiti wa kijiji hicho, Makwaiya Mwandu, alithibitisha kukosekana kwa maji safi na salama kijijini kwao.

Mwandu, alisema hali hiyo imekuwa ikiwalazimika kutumia maji ya kwenye bwawa hilo kwa ajili ya kunywa, kupikia na usafi.

Meneja wa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Shinyanga (RUWASA) Mkoa wa Shinyanga, Julieth Payovela, alisema wanatarajia kupeleka kijijini hapo kutoka Ziwa Victoria ambao utagharimu zaidi ya Sh.milioni 381.

Julieth, alisema mradi huo unaendelea kutekelezwa katika Kata ya Itilima baada ya kukamilika awamu ya kwanza utahudumia vijijini vya Ipeja, Ikonokelo na Ikome na Itilima kitapata maji awamu ya pili.

Alisema kazi zisizo za ujuzi kipaumbele kinatolewa kupewa vijana wanaoishi vijiji ambako mradi huo unapita na kuwataka wananchi kuwa wavumilivu wakati serikali ikiendelea kutatua tatizo la ukosefu wa maji vijijini ili kila kimoja kipate huduma hiyo.



Mbunge wa Jimbo la Kishapu, Boniphace Butondo (kushoto), akiwa na mke wake, Eva Ndamo katika hafla ya kusimikwa kuwa Mtemi wa Buduhe, wilayani Kishapu, mkoani Shinyanga juzi, ambaye atakuwa Nyangindu wa tatu. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Raia wa nje marufuku daftari la wakazi

**Na Waandishi Wetu**

VIONGOZI wa mikoa na wilaya mkoani Shinganya na Mwanza wameongoza wananchi kujiandikisha katika daftari la wakazi kwa ajili ya uchaguzi wa serikali za mitaa na kupiga marufuku raia wa nje kushiriki kwani ni kinyume cha sheria.

Miongoni mwao ni Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha ambaye juzi baada ya kujiandikisha katika viwanja vya Ikulu Manispaa ya Shinyanga, akiwa ameambatana na Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Julius Mtatiro alisisitiza kuwa ni marufuku raia hao wa nje kujiandikisha katika daftari hilo kwa ajili ya kushiriki katika uchaguzi huo utakaofanyika nchini mwezi ujao.

"Naagiza kamati ya ulinzi na usalama, maofisa uandikishaji na wa Idara ya Uhamiaji kuhakikisha wanafanya ufuatiliaji wa kina ili kutoandikisha kwenye daftari la wakazi watu ambao siyo raia wa Tanzania," alisema Macha.

Aliwataka wakazi mkoani hapa, wakiwamo wanawake na vijana wenye sifa kujitokeza kwa wingi kuwania uongozi katika uchaguzi huo wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji kwa kuwa ni haki yao ya msingi kikatiba.

Alisema zaidi ya watu milioni 1.1, wanatarajiwa kuandikisha katika vituo 2,941 mkoani hapa kwa ajili ya kuchagua viongozi wao.

Katika hatua nyingine; Mkuu wa Wilaya ya Sengerema mkoani Mwanza, Senyi Ngaga akizungumza baada ya kujiandikisha katika daftari hilo, alitoa wito kwa wakazi wilayani humo kujitokeza kuchagua viongozi bora katika uchaguzi huo ili wawaletee maendeleo kwenye maeneo yao.

Wakala wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Said Kibuya, alisema uandikishaji katika daftari hilo unaendelea vizuri, huku akisisitiza hamasa iongezwe zaidi ili wananchi waendelee kujitokeza kwa wingi.

Baadhi ya wakazi wilayani humo waliahidi kwenda kujiandikisha kwani ni haki yao ya msingi kuchagua viongozi wanaowataka.

***Imeandaliwa na Marco Maduhu (SHINYANGA), Elizabeth Seleman (SENGEREMA)***

## Wafanyabiashara wataka uwezeshwaji kiuchumi

**Na Restuta Damian,** KAGERA

BAADHI ya wafanyabiashara mkoani hapa wameiomba serikali kukuza mitaji kwa ajili ya wanawake, vijana na wenye uhitaji ili kukuza uchumi.

Walisema hatua hiyo itawasaidia kutunza faida wanayopata katika biashara zao badala ya kukuza mitaji na kujikuta wakishindwa kuendeleza biashara zao.

Wakizungumza juzi kwa nyakati tofauti Nipashe baada ya kushiriki Programu ya Uimalishaji wa Uchumi na Mama Samia, kupitia Baraza la Taifa la Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi (NEEC), mjasiriamali kutoka Kisiwa cha Goziba, Advera Raulent, alisema matarajio yao ni wanawake kuwa na mitaji ili kupanua biashara zao.

Advera, alisema ukosefu wa mitaji unasababisha warudi nyuma kwa maendeleo wakati walikuwa wamefika hatua ya kutambuliwa na wateja.

"Tayari wanawake wemeonesha nia ya kujituma, wamebuni biashara na kupata soko, kinachokwamisha ni mtaji kufikia wateja maradufu," alisema.

Mfanyabiashara wa nafaka katika Soko la Bukoba, Prospa Clement, alisema tatizo la ukosefu wa mitaji na maarifa ya biashara, yanawakumba wengi wao kwa kukosa elimu ya ujasiriamali.

Alishauri mikopo inapotolewa iambatane na elimu hiyo ili kuboresha biashara baada ya kuelimishwa jinsi ya kukuza mitaji.

Mratibu Jukwaa hilo, Mkoa wa Kagera, Issa Mulimi, alisema mkoa huo una fursa za kilimo kwa mazao ya nafaka na mizizi.

Kwa mujibu wa Mulimi, jukwaa hilo limesajili vikundi 3,492 vya wanawake, vijana na wenye uhitaji kupitia ngazi ya vitongoji, vijiji, kata na halmashauri.

"Mkoa umepanga kutoa kiasi cha Sh. bilioni 5.9 zitakazogawanywa kwenye halmashauri nane ili kutoa mikopo kwa makundi haya," alisema.


Alisema kwa Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo zitatolewa zaidi ya Sh.milioni 700, Karagwe Sh.milioni 300, Ngara Sh.milioni 400, Bukoba Sh. milioni 500, Muleba Sh.bilioni 1.8, Manispaa Sh. milioni 600, Missenyi Sh. bilioni moja na Kyerwa Sh. milioni 400.

Katibu Mtendaji NEEC, Beng'i Issa, alitaja moja ya majukumu ya programu hiyo ni kufanya vipimo vya mafanikio ya wananchi kutokana na wengi kukosa ufahamu wa fursa zinazopatikana serikalini.



Ukurasa 13

**MTOTO WA KIKE DUNIANI**
**Wadau wanapoibua ya muhimu kumwandaa binti kuwa kiongozi**



Ukurasa 14

**Naibu Rais Kenya hatima yabaki 'kwa maseneta'**



AKIBA YA DHAHABU BOT

# Taifa linajihakikishia utulivu na uthabiti wa sarafu

**Na Gaudensia Mngumi**

RAIS Samia Suluhu Hassan, ametangaza kuwa Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imetenga Shilingi trilioni moja kwa ajili ya kununua dhahabu kwa lengo la kuwa na akiba kubwa zaidi ambayo ni dhamana ya utajiri wa taifa kwa miaka ijayo.

Ni tangazo analolitoa kwenye maadhimisho ya kumbukumbu ya miaka 25 ya kifo cha Baba wa Taifa Hayati Mwalimu Julius Nyerere mkoani Mwanza wiki hii.

Dhahabu tangu mwanzo ni utajiri na mali muhimu kwa karne nyingi na kwa hivyo, akiba ya dhahabu hutumika kama kiashiria cha utajiri ulio ndani ya taifa. Kwanza ni njia ya kudhibiti na kuimarisha thamani ya sarafu ya nchi wakati wa kuyumba kwa soko, na hivyo kuuhakikishia uchumi utulivu na uthabiti.

Uamuzi wa serikali wa kuanzisha hifadhi ya dhahabu Benki Kuu kama inavyosisitizwa na Rais Samia ni hatua muhimu ya kupongezwa na inayotazama mbele kuelekea uwezeshaji na uimarisha wa uchumi wa nchi, anasema Dk. Peter Kafumu, Kamishna wa Madini mstaafu.

Anaeleza katika mahojiano na Nipashe kuwa kuanzishwa kwa hifadhi ya dhahabu ya Tanzania kutakuwa nguzo msingi kulinda fedha za ndani.

Aidha, kuweka utulivu wa sarafu, kufanya malipo, kuvutia fedha za kigeni, kuimarisha pia imani ya wawekezaji na kutoa kinga kwa sekta ya fedha dhidi ya mabadiliko ya kiuchumi duniani." Anafafanua Dk. Kafumu ambaye amewahi kuwa mbunge wa Igunga na kuzungumzia umuhimu wa kuwa na akiba hiyo.

Dk. Kafumu mtaalamu wa jiolojia na madini, anasema Tanzania yenye akiba kubwa ya dhahabu, itaimarisha imani ya kimataifa katika uthabiti wake wa kiuchumi na uwezo wake wa kukopeshwa na kuvutia uwekezaji zaidi kutoka nje (DFI) ambao nao utavutia fedha nyingi za kigeni kuingia nchini.



Gavana wa Benki Kuu, Dk. Emmanuel Tutuba. **PICHA MTANDAO**

Anasema hifadhi hiyo huvutia pesa nyingi za kigeni, aidha inaimarisha thamani ya Shilingi na pale nchi inapouza bidhaa nyingi nje zaidi kuzidi inavyoagiza, kwa kawaida hupokea fedha za kigeni, ambazo zinaimarisha sarafu yake ya ndani.

Kinyume chake, ikiwa inaagiza zaidi bidhaa kutoka nje inamaanisha fedha za kigeni hupungua na kuishusha thamani. Katika suala hilo, akiba yenye nguvu ya dhahabu inatoa kinga dhidi ya nakisi ya kibiashara na misukosuko ya kiuchumi ndani ya nchi.

Akizungumzia hatua hiyo, mtaalamu wa masuala ya uchumi (jina linahifadhiwa) anasema utaratibu wa kuwa na akiba ya dhahabu ni muhimu kiuchumi, kwa maelezo kwamba nchi inapokosa fedha za kigeni, inaingiza dhahabu sokoni na kupata fedha hizo kuendesha miradi ya maendeleo.

Anafafanua kuwa mara nyingi soko la dhahabu haliyumbi kama ilivyo kwenye bidhaa nyingine, ndiyo maana mataifa kama Marekani, Ujerumani Afrika Kusini, Urusi, Uingereza na India zinatunza madini hayo ili kusimamia sarafu za kuuza pale upungufu unapotokea.

"Nchi yenye dhahabu ni tajiri, ndiyo maana wenzetu hao wa mataifa makubwa wanatunza dhahabu ya kutosha kwani zinajua umuhimu wake," anaongeza.

Anafafanua kuwa hatua iliyochukuliwa na BoT ya kununua dhahabu zaidi na kuongeza akiba ni wazi inatambua umuhimu na nguvu ya dhahabu katika maendeleo ya nchi.

Hata hivyo, anasema ili utaratibu huo uweze kuwa matokeo mazuri, ni muhimu serikali kudhibiti masoko holela ya dhahabu ambayo yanaweza kukwamisha kile ambacho BoT inakusudia.

"Nikumbushe kuwa si mara ya kwanza BoT kutunza dhahabu ya ziada, iliwahi kufanya, hivyo kisha ikaachana na utaratibu baada ya kubaini kuwa kulikuwa na kasoro.

"Kama safari hii serikali imejipanga ni vyema kudhibiti dhahabu inayonunuliwa ili iwe halisi na kusiwe na upungufu ili taifa liwe kama mataifa makubwa kwa kuimarisha uchumi, kutokana na ukweli kwamba soko la dhahabu haliyumbi," anasema.

Mtandao wa GlobalData, unaeleza kuwa Tanzania ni nchi ya 18 kwa uzalishaji wa dhahabu duniani kwa mwaka jana, wakati mchimbaji mkuu Afrika ni Ghana, ikifuatiwa na Afrika Kusini, Sudan, Mali na Tanzania pia ni mdau mkuu katika sekta ya dhahabu ukanda wa Afrika Mashariki.

Mitandao inaeleza kuwa akiba hiyo inayotunzwa na benki kuu ya nchi ni utajiri wa taifa, unaoohifadhiwa kwa namna ya matofali (ingots) ya dhahabu, ambayo hata serikali 'ikichacha 'kufilisika' dhahabu huuzwa na kupata fedha za kuendesha uchumi.

Akiba hiyo inahifadhiwa na benki kuu kwa lengo la kuwa kama dhamana ya kusimama iwapo kuna madeni lakini pia kulipa inapohitajika kufanya hivyo. Kwa ujumla Tanzania inachokusudia kufanya ni kama kuwa ghala la 'thamani' la kusaidia kuongeza nguvu thamani ya sarafu ya taifa ambayo ni Shilingi ya Tanzania. Ni kuipa nguvu zaidi na kuiwezesha kusimama kidete.

INAENDELEA UK. 12

# FRELIMO yaibuka kidedea RENAMO, wapinzani wenza watupwa mbali

**Na Christina Mwakangale**

MGOMBEA Daniel Chapo, wa chama kikongwe cha siasa Msumbiji cha FRELIMO, ameshinda kiti cha urais katika majimbo mengi makubwa ya nchi hiyo pamoja na mji mkuu Maputo.

Baada ya kutawala Msumbiji tangu uhuru mwaka 1975, kimetawala miaka 50, kilielezwa kuzoa asilimia 53.68 ya kura zilizopigwa Maputo. Mwingine ni Venâncio Mondlane mtoto wa mpigania uhuru Edward Monndlane, akipata asilimia 33.84, akifuatiwa na Ossufo Momade wa RENAMO, aliyepata takriban asilimia tisa wakati Lutero Simango wa chama cha MDM akiwa na asilimia tatu.

Itakumbukwa kuwa Eduardo Mondlane alikuwa mwanamapinduzi na mwanaharakati wa ukombozi wa Msumbiji, ambaye ni mwanzilishi wa Chama cha Ukombozi cha Msumbiji FRELIMO. Alikuwa kiongozi wa kwanza wa FRELIMO hadi alipouawa mwaka 1969 nchini Tanzania na wapinga ukombozi wa Afrika.

FRELIMO ni miongoni mwa vyama vikongwe barani Afrika na kimedumu mamlakani kwa takribani nusu karne.

Upinzani umepinga matokeo hayo katika maeneo yalikotangazwa hasa majimbo makubwa baada ya uchaguzi mkuu uliofanyika wiki iliyopita Oktoba 9.

Nickson Katembo, mchambuzi wa kisiasa akiwa nchini humo anasema wananchi walio wengi hawakutarajia matokeo hayo. Chapo kupitia FRELIMO katika uchaguzi huu, amegombea akimrithi Rais anayemaliza muda wake, Filipe Nyusi.

Mpinzani wake mkuu ni Ossuo Momade, kutoka RENAMO, wengine walikuwa ni Lutero Simango wa MDC na mgombea binafsi Venâncio Mondlane.

Kwa mujibu wa Tume ya Uchaguzi ya Taifa (CNE), zaidi ya watu milioni 17 walijiandikisha kupiga kura, wakiwamo 333,839 wanaoishi nje ya nchi.

FRELIMO, ilishinda kwa kura nyingi katika uchaguzi mkuu wa urais wa mwaka 2019 baada ya kupata asilimia 73 ya kura zilizopigwa, japo RENAMO, ilitupilia mbali ushindi huo kwa madai ya kukosa imani na mchakato wote.





Mshindi wa urais Msumbiji Daniel Chappo wa FRELIMO (kushoto) na mgombea huru asiyefungamana na chama chochote kwenye urais huo, Venancio Mondlane. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

Kwa mujibu wa Radio DW, bado hakuna matokeo rasmi, lakini inadhihirika wazi kuwa FRELIMO, chama kilichokuwa madarakani tangu uhuru mgombea wake, Chapo, atashinda.

Katika kinyang'anyiro cha urais, Mondlane, mmoja wa wagombea watatu wa upinzani aliondoka RENAMO na kuwania kama mgombea binafsi, dhidi ya mwenyekiti wa RENAMO, Ossufo Momade.

Mondlane anadai ni mwathirika wa udanganyifu mkubwa katika uchaguzi: "Tunachokiona hapa ni wizi wa hali ya juu kabisa wa uchaguzi," anaiambia DW na kuongeza: "Hili si jambo jipya, tumeona hili chaguzi zilizopita."

Katika eneo lenye utulivu la kaskazini mashariki la Cabo Delgado, ambalo limevumilia vita vya umwagaji damu vya wanajihadi tangu 2017, Chapo pia alishinda rasmi, kwa takriban asilimia 66 ya kura, akifuatiwa na Mondlane asilimia 22.64.

Momade alishika nafasi ya tatu kwa asilimia 7.56 na Lutero Simango alimalizia mwisho, kwa chini ya asilimia nne.

"PODEMO, chama ambacho bado hakijawakilishwa bungeni ambacho kilimuunga mkono Mondlane kuwania urais, kitachukua nafasi ya RENAMO," mchambuzi wa Msumbiji Jaime Guiliche aliiambia DW.

"Nadhani tutaona hali ambayo Renamo si tena nguvu ya pili kwa ukubwa wa kisiasa na itaanguka hadi nafasi ya tatu. Hiyo ingekuwa mabadiliko makubwa katika mazingira ya kisiasa ya nchi yetu," Guiliche anasema.

Uchaguzi mkuu wa Jumatano ulijumuisha uchaguzi wa saba wa kiti cha urais kwa nchi hiyo, Rais Filipe Nyusi, amefikia kikomo cha kikatiba cha mihula miwili, hajashiriki.

Kwa mujibu wa sheria ya uchaguzi, matokeo ya majimbo yanapaswa kuhesabiwa hadi mwisho wa leo, huku hesabu katika wilaya zote 154 za nchi ikiwa imekamilika mwishoni mwa wiki.

Kwa matokeo hayo ambako tayari yametangazwa, hakuna duru ya pili, huchukua hadi siku 15 (kuhesabiwa tangu kufungwa kwa kura), kabla ya kupitishwa kuthibitishwa na Baraza la Katiba, ambalo hakuna tarehe ya mwisho ya kutangaza matokeo rasmi baada ya kuchanganua rufani zinazowezekana.

Kura hiyo ilijumuisha uchaguzi wa wabunge wa bunge la kitaifa (manaibu 250) na wa mabunge ya majimbo na magavana wao husika na viti 794 vitagawanywa.

*Club of Mozambique*

## TAIFA LINAJIHAKIKISHIA UTULIVU NA UTHABITI WA SARAFU

**INATOKA UK. 11**

Licha ya Tanzania kuzalisha dhahabu, ujio wa hifadhi hiyo ni kitu hicho hakijawahi kuwapo na kwa sasa kujengwa akiba ya madini hayo BoT ni historia ambayo taifa litaandika sasa.

**HIFADHI KUBWA DUNIANI**

Mitandao inaonyesha kwamba Benki Kuu ya Marekani ndio ya kwanza duniani kwa kuweka hazina kubwa zaidi ya dhahabu inatunza tani 8,133.46. Kadhalika, Benki ya Bundesbank au Benki Kuu ya Ujerumani, imehifadhi tani 3,352.65 za dhahabu, ambayo ni pungufu ya kiwango kilichoko kwenye benki kuu ya Marekani.

Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) nalo linamiliki akiba kubwa ya dhahabu lina tani 3,102.01. Nchi nyingine ni Italia, ambayo ilianza kukusanya dhahabu miaka zaidi ya miaka 131 iliyopita ikimaanisha kuwa jukumu hilo lilianza mwaka 1893 na leo ina tani 2,452

Taifa jingine ni Ufaransa yenye tani 2,437, Urusi 2,336, China 2,264, Uswizi 1,040 , Japan 846, India 831 na Uholanzi 612.

Kwa vile dhahabu ni kitu halisi, ni chanzo cha kuwa na uhakika na uaminifu kifedha katika nchi, na katika mazingira yote ya kiuchumi na kuifanya kuwa mojawapo ya rasilimali muhimu zaidi za hifadhi ya kiakiba ya fedha duniani kote.

Kwa kulinganisha Dola ya Marekani na dhahabu dola inaposhuka thamani, dhahabu inapanda hivyo kuwezesha benki kuu kulinda akiba zake wakati wa misukosuko na kuyumba kwa soko na hata thamani za fedha.

Kwa Afrika mataifa wazalishaji wakubwa wa dhahabu kama Ghana wana akiba ya madini hayo na taarifa za mitandao zinaonyesha kuwa taifa lenye kiwango kikubwa cha akiba ya dhahabu kinapatikana Algeria yenye tani 174, inafuatiwa na Libya 147, Misri 127, Afrika Kusini 125, Morroco 22, Nigeria 21, Mauritus 12, Ghana 8.7, Tunisia 6.84, Msumbiji 3.9, Malawi 0.4, Burundi 0.08 na Kenya 0.02.

Hatua hiyo ya kutangaza kuimarishwa hifadhi ya dhahabu BoT ni ya kijasiri na inaweza kukabiliana na mashaka ya kuyumba kwa thamani ya sarafu.

MTOTO WA KIKE DUNIANI

# Wadau wanapoibua ya muhimu kumwandaa binti kuwa kiongozi

NA SABATO KASIKA

MAADHIMISHO ya Siku ya Kimataifa ya Mtoto wa Kike Duniani mwaka huu, yamefikia kilele wiki iliyopita Oktoba 11, yakiwa na kaulimbiu 'mtoto wa kike na uongozi, tumshirikishe wakati ni sasa'. Ili kufanikisha kaulimbiu hiyo, Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), unakuja na hoja tano ambazo unaamini zikifanyiwa kazi zinaweza kusaidia kumwandaa mtoto wa kike kuwa kiongozi wa baadaye.



Halima Masoud akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Msingi Mji Mpya. **PICHA: SABATO KASIKA**

Akiwasilisha salamu za TGNP katika maadhimisho hayo yaliyofanyika kwenye viwanja vya Shule ya Msingi Mji Mpya jijini Dar es Salaam, msimamizi wa klabu za kupinga ukatili shuleni kutoka Kituo cha Taarifa na Maarifa Majohe ambacho kiko chini ya mtandao huo, Halima Masoud, anataja hoja ya kwanza kuwa ni elimu.

Anasema elimu ni msingi wa kumjenga mtoto wa kike ili awe kiongozi bora wa kesho, na kwamba anapopewa elimu bora anakuwa na fursa nyingi za kuchangia maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

"Elimu humfanya mtoto wa kike awe na uwezo wa kufanya maamuzi ya busara na kuwa sauti ya mabadiliko katika eneo lake," anasema Halima kwa niaba ya uongozi wa TGNP.

Msimamizi huyo wa klabu za jinsia anataja hoja ya pili kuwa ni kujadili jinsi ya kuondoa vikwazo vya kijinsia vinavyomzuia mtoto wa kike kupata fursa za uongozi, hasa jinsi ya kupambana na mila potofu na mitazamo ya kijamii inayombagua mtoto wa kike.

"Hoja ya tatu ni kwamba, tunapaswa kumfundisha mtoto wa kike jinsi ya kujitambua, kujisimamia na kuwa na ujasiri wa kuongoza. Uongozi unataka kujiamini, ni jukumu letu kuhakikisha watoto wa kike wanapata mazingira yanayowasaidia kukuza sifa hizi," anasema.

Akizungumzia hoja ya nne, anasema inahusu mitandao ya kijamii, kwamba inaweza kutumika kama chombo cha kuwaongezea watoto wa kike uelewa kwa kuwa ina vitu vingi vya kujifunza kuhusu uongozi na kuleta mabadiliko.

"Watoto wa kike pia wanatakiwa kufundishwa kutumia majukwaa hayo kuhamasisha na kushirikiana na wengine katika masuala mbalimbali ya kijamii," anasema.

Katika hoja ya tano, Halima anasema watoto wa kike wanatakiwa kupewa fursa kwa vitendo, kwa kuwajengea mazingira yanayowawezesha kujifunza ujuzi wa uongozi kwa vitendo.

"Hii inamaanisha kuwashirikisha katika shughuli za shule, kijamii na hata taasisi ili waweze kujifunza kwa vitendo na kupata uzoefu mapema wangali wadogo," anasema.

### MAJUKUMU YA KLABU

Halima anasema kwa kushirikiana na uongozi wa msingi na sekondari katika kata hiyo, wamefanikiwa kuanzisha klabu za jinsia shuleni ili kusaidiana wanafunzi wa kike kupata fursa ya kuzungumza masuala yanayowahusu na kujieleza bila woga.

Anasema wameanzisha klabu za jinsia katika shule za msingi tano za Viwege, Mji Mpya, Kichangani, Majohe na Uamuzi, na kwamba kila shule imejipangia siku ya wanafunzi kukutana katika klabu hizo ili kujadili mambo yanayowahusu na kuweka mikakati ya kuyatatua.

Mfano, watoto wa kike wanakabiliwa na changamoto nyingi za ukatili ukiwamo wa kukeketwa na kubakwa, hivyo kupitia klabu zao wanakuwa huru kueleza tatizo hilo kwa mwalimu wao wa klabu," anasema.

Mwalimu wa klabu ya jinsia wa Shule ya Msingi Mji Mpya, Mary Kwingwa, anasema kila Jumatano wanafunzi wa klabu hiyo hukutana na kueleza changamoto zao.

"Huwa wanafunguka mambo mengi ambayo nasi huyachukua na kuyafanyia kazi yale ambayo yako ndani ya uwezo wetu, kama ni makubwa, tunayafikisha kwa wazazi, walezi au kwa viongozi wa serikali ngazi ya mtaa," anasema Mary.

Mary anafafanua kuwa kupitia klabu ya jinsia shuleni hapo, kumekuwa na mwamko mkubwa wa wanafunzi wa kike kujieleza bila woga na kwamba hiyo ni njia mojawapo ya kuandaa mtoto wa kike kuwa kiongozi wa baadaye.

Anasema awali kulikuwa na matukio mengi ya ukatili wa kijinsia kwa wanafunzi, uliokuwa ukifanywa na baadhi ya watu wa mitaani huku taarifa zikifichwa, na kwamba sasa umepungua.

"Tumewafundisha watoto jinsi ya kutoa taarifa za matukio hayo kwa kushirikiana na Kituo cha Taarifa na Maarifa Majohe, sasa kukiwa na viashiria vya vitendo, wanatoa taarifa kwetu," anasema.

Mmoja wa wanafunzi hao, Mwajuma Ally anayesoma darasa la tano, anasema klabu hiyo inaweka mazingira ambayo yanampa fursa mtoto wa kike kujifunza uongozi kwa vitendo.

"Miongoni mwa fursa hiyo ni kutushirikisha katika shughuli za shule, kwani tunajifunza kujitambua, kujisimamia na kuwa na ujasiri wa kuongoza. Ninaipenda klabu yetu ya jinsia," anasema Mwajuma.

Mwalimu mkuu wa shule hiyo, Abubakar Shauri, anasema shule hiyo ilikuwa na wanafunzi 3,131, lakini sasa wamebaki 2,497 baada ya wengine wa darasa la saba kufanya mtihani wa taifa.

"Penye wingi wa wanafunzi kama hao kuna mambo mengi, hivyo kuanzishwa kwa klabu kumesaidia kwenye baadhi ya mambo ambayo tulikuwa hatuyajui, lakini sasa tunayajua," anasema Shauri.

Anataja baadhi ya mambo hayo kuwa ni baadhi ya watoto kutoroka shule wakati wa masomo kutokana na kwamba shule haina uzio, na kuongeza kuwa klabu imesaidia kuwaumbua wenye mtindo huo.

"Tatizo limepungua kwa sababu kupitia klabu yao, wanasaidia kuwabaini wanaotoroka na kufikisha majina yao kwa walimu, kwa ajili ya hatua zaidi za kinidhamu," anasema.

Aidha, mwalimu mkuu huyo anasema sasa anaendelea na mikakati kutafuta wadau ili kupata fedha za kuweka uzio ili kuzuia vijana wa kihuni kupita katika mazingira ya shule.



Mwalimu wa klabu ya jinsia wa shule hiyo, Mary Kwingwa, akisoma taarifa kuhusu maadhimisho hayo mbele ya wanafunzi, huku Mwalimu Mkuu Abubakar Shauri akishuhudia. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Naibu Rais Kenya hatima yabaki 'kwa maseneta'

## •Wako 57, ikitokea 45 wakamkataa ametumbuliwa

Na Christina Mwakangale

NAIBU Rais wa Kenya, Rigathi Gachagua (husomwa Gashagwa), baada ya kuzunguka Kenya nzima akimpinga mgombea aliyeandaliwa na Uhuru Kenyatta-Raila Odinga, na kufanikisha ushindi wa William Ruto, sasa anavuna alichopanda. Ni sawa na kusema anapokea shukurani ya punda ambayo ni mateke.

Anapata asante hiyo kwa vile uhusiano wake na Rais Ruto umetibuka na sasa amekali kuti kavu akiondolewa kwenye nafasi hiyo.

Matumaini ya kusalia katika uongozi yako mikononi mwa jopo la majaji watatu. Ingawa msimamo wake ni kwamba, kosa lililoonekana kwake linamhusu pia Ruto, akieleza walichaguliwa kwa pamoja.

Jaji Mkuu Martha Koome, Jumatatu wiki hii ameteua jopo la majaji watatu, ili waamue kesi sita ambazo ziliwasilishwa kupinga mchakato wa kumwondoa Gachagua.

Tangu aondolewe na Bunge la Kitaifa wiki iliyopita, amezungumza kwa mara ya kwanza hadharani, mbunge huyo wa zamani wa Mathira akielezea kuwa mahakama itashughulikia suala lake.

Awali alilitaka Bunge la Kitaifa, kuheshimu chaguo la wananchi akisema walichaguliwa kwa tiketi moja na Rais Ruto na hivyo haifai alengwe kutumbuliwa.

Jaji Koome amewateua majaji Eric Ogola, Anthony Mrima na Dk. Freda Mugambi kusikiliza kesi hizo sita, ikiwamo moja ambayo iliwasilishwa na Gachagua mwenyewe.

Katika uamuzi wake Ijumaa iliyopita, Mahakama Kuu ilikubaliana na mawakili wa Gachagua wakiongozwa na Paul Muite, kuwa masuala sita ambayo yaliibuliwa, yaliyokuwa na uzito yalikuwa ya kikatiba.

"Ikizingatiwa kuwa kesi hizo zinafuatiliwa sana na umma kwa sababu naibu rais wa nchi ameondolewa mamlakani, ni uamuzi wangu kuwe na jopo litakaloangazia mchakato uliofuatwa iwapo unawiana na katiba au la," akaamua Jaji Mugambi.

Kati ya masuala ambayo yatazingatiwa ni kanuni za Bunge la Kitaifa, ambazo zilitumiwa kumtimua Gachagua. Naibu Rais alisema kanuni hizo ziliweka siku 12 pekee kukamilisha mchakato wa kumtimua, siku ambazo ni chache zaidi.

Gachagua pia anadai kutolewa kwa siku hizo chache kulisababisha mikutano ya ushirikishaji wa umma kuharakishwa na raia kutoshirikishwa vilivyo jinsi katiba imeamrisha.

Muite pia alisema Bunge la Kitaifa liliegemea upande mmoja katika mchakato huo wa kumtimua naibu rais. Bunge lilijitetea likisema naibu rais alipewa muda wa saa mbili kujitetea mbele ya wabunge.

Jaji huyo alisema kuwa ni haki kwa raia kufahamu iwapo sheria za sasa zinawapa muda mwafaka wa kushiriki vyema mchakato wa kumwondoa Naibu Rais.

Jumanne (jana asubuhi), Jaji Chacha Mwita ametoa uamuzi iwapo mahakama itazuia Bunge la Seneti kujadili na kuipigia kura hoja ya kumtimua Gachagua ambayo ilipitishwa na Bunge la Kitaifa.

### HATIMA YAKE

Naibu Rais Gachagua, sasa anategemea Mahakama imwokoe maseneta wanapoanza kuchambua hoja ya kumwondoa ofisini.

Gachagua ambaye amekuwa akisimama kidete wakati huu ambako kuna dhoruba ya kisiasa ikimkabili, mwishoni mwa wiki, alielezea kuwa matakwa ya wananchi hayawezi kubatilishwa na mawakilishi wachache.

Akiongea hadharani tangu wabunge walipopitisha hoja ya kumbandua, alilitaka bunge kuheshimu chaguo la wananchi akisema alichaguliwa kwa tiketi moja na Rais Ruto.

Akipongeza Idara ya Mahakama kwa kuzingatia haki wakati wa kufanya maamuzi yake, Gachagua anasema mhimili huo utaheshimu matakwa ya wananchi akiongeza kuwa: "Nchi nzuri huendeshwa kwa misingi ya heshima kwa utawala wa kisheria."

"Naheshimu uhuru wa Idara ya Mahakama. Nina uhakika kuwa mahakama zitadumisha uhuru wake, kulinda katiba na matakwa ya wananchi," anasema Gachagua.

"Mahakama zetu hufanya kazi vizuri. Majaji hulinda Katiba, utawala wa sheria na daima huhakikisha matakwa ya wananchi yanaheshimiwa. Nina uhakika kuwa utawala wa sheria utazingatiwa na matakwa ya wananchi kudumishwa," akaongeza.

Gachagua alikuwa akiongea katika Ibada ya Jumapili katika Kanisa la Kianglikana (ACK), Dayosisi ya Embu, wakati wa maadhimisho ya miaka 34 tangu kuanzishwa kwa dayosisi hiyo.

Huku akiwasifu wabunge 44 waliopiga kura ya kupinga hoja hiyo iliyodhaminiwa na Mbunge wa Kibwezi Magharibi, Mwengi Mutuse, Naibu Rais aliwahimiza viongozi kusikiliza matakwa ya raia.

Aliwasihi Wakenya wamwombee na taifa pia wakati ambao joto la kisiasa limepanda, baada ya wabunge kupitisha hoja ya kumtimua wiki jana.

Vile vile, aliwataka Wakenya kusalia watulivu pasina kujadili matokeo ya uamuzi wa Seneti kuhusu hoja hiyo.

Gachagua ambaye alikuwa ameambatana na mkewe Dorcas Rigathi, hata hivyo alisema yuko tayari kwa uamuzi wowote kutoka kwa Seneti.

Pia, aliongozana na viongozi kadhaa akiwamo Mbunge wa eneo hilo (eneo bunge la Manyatta) Gitonga Mukunji, Mbunge Mwakilishi wa Embu Pamela Njoki Njeru, almaarufu Doubl N.

Wengine ni Onesmus Ngogoyo (Kajiado Kaskazini), James Gakuya (Embakasi Kaskazini), George Koimburi (Juja), Seneta wa Kirinyaga Kamau Murango, aliyekuwa Mbunge Mwakilishi wa Laikipia Cate Waruguru na madiwani.

Jumatano (leo), Bunge la Kitaifa, likiongozwa na Mutuse (Mbunge wa Kibwezi Magharibi), litawasilisha kesi yake mbele ya Seneti majira ya adhuhuri.

Bunge hilo litawasilisha ushahidi wake na mashahidi hadi saa kumi na nusu jioni. Kisha mawakili wa Gachagua watawahoji mashahidi hao kwa saa mbili hadi saa kumi na mbili na nusu jioni.

Baadaye, Maseneta watapewa muda wa saa moja kuwauliza maswali na kusaka ufafanuzi kabla ya shughuli za siku hiyo ya kwanza kutamatishwa.

Mutuse na Bunge la Kitaifa watawatumia Gavana wa Nairobi Johnson Sakaja, Katibu katika Baraza la Mawaziri Mercy Wanjau na aliyekuwa Kaimu Ofisa Mkuu Mtendaji wa KEMSA, Andrew Mulwa kama mashahidi wao.

Gachagua atawakilishwa na jopo la mawakili wakiongozwa na Wakili Mkuu, Paul Muite.

Wengine ni pamoja na Victor Swanya, George Wandati, Faith Waigwa, Elisha Ongoya, Ndegwa Njiru, George Sakimpa, Murigi Kamande, Amos Kisilu, Tom Macharia na Julia Omwamba.

Kwa upande mwingine Bunge la Kitaifa pia limekodi huduma za jopo la mawakili likiongozwa na Wakili Mkuu, Paul Nyamodi.

Nyamodi atasaidiana na akina Eric Gumbo, Kipkogei Moses Kipkemboi, Muthomi Thiankolu, Peter Wanyama, Melly Kennedy Kipkoech, Joan Jeruto, Muriuki Eric Mwirigi, Mwereru Boniface Mawira na Ondago Kevine Otieno.

Gachagua anakabiliwa na mashtaka 11 ikiwamo kukaidi uamuzi uliopitishwa katika baraza la mawaziri la kuwafurusha watu waliojenga makazi ndani ya eneo la mita 30 kutoka kingo za mito katika kaunti ya Nairobi.

Kwa kufanya hivyo, Naibu Rais alikiuka kanuni ya uwajibikaji wa pamoja wa wanachama wa Baraza la Mawaziri.

Pia anakabiliwa na tuhuma ya kuingilia mipango ya serikali ya kaunti ya Nairobi ya kuwahamisha wafanyabiashara kutoka soko la wakulima hadi soko jipya lililoko katika Barabara ya Kangundo, eneo la bunge la Embakasi Mashariki.

Kesho Alhamisi, asubuhi itakuwa zamu kwa Naibu Rais kujitetea dhidi ya mashtaka yote yaliyoelekezwa dhidi yake na Bunge la Kitaifa.

Katika wasilisho litakaloanza saa 3:00 asubuhi, Gachagua atawasilisha ushahidi, hati ya kiapo na mashahidi hadi saa 7:00 mchana.


Inasemekana kuwa Naibu Rais atawasilisha mashahidi kadhaa lakini mawakili wake wamegoma kufichua majina na idadi yao.

Saa moja itatengwa ya kuhojiwa kwa mashahidi wa Gachagua, shughuli itakayoendelea hadi saa tisa na nusu alasiri.

Baada ya hapo Maseneta watapewa muda wa saa moja kuuliza maswali na kupata ufafanuzi.

Saa mbili zitatengewa taarifa za mwisho kutoka pande mbili kabla ya mjadala kamili kuanza kuanza saa 12:30 jioni.

Gachagua atakuwa ameondolewa ofisini rasmi, ikiwa angalau Maseneta 45 kati ya 57 watapiga kura kuidhinisha mojawapo kati ya mashtaka 11 dhidi yake, ambayo awali ndiyo sababu ya kilichomwondoa kupitia Bunge la Kitaifa.



Ni kitimoto kati ya Rais William Ruto (kulia) na Naibu Rigathi Gachagua. **PICHA: MTANDAO**



## HABARI DODOMA

## ‘Wanafunzi jiepusheni dawa za kulevya’

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WANAFUNZI mkoani hapa, wametakiwa kujiepusha na matumizi ya dawa hizo ili kutimiza ndoto zao kwa kupata elimu na kuwa wataalamu kwa siku zijazo.

Kamishna Msaidizi wa Mamlaka ya Dawa ya Kulevya Kanda ya Kati, Mzee Kasui, atoa wito huo jana jijini hapa kwenye mdahalo wa shule za msingi ulioandaliwa

na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Dodoma wenye lengo la kutoa elimu ya kupinga rushwa na matumizi ya dawa za kulevya kwa vijana.

Aliwahimiza wanafunzi hao kujiunga na klabu za kupinga rushwa ili kuepuka vitendo vya kuomba, kutoa na kupokea rushwa kwa kuwa vina athari kubwa kwa taifa.

Alisema matumizi ya dawa hizo ni tatizo kubwa kwa vijana, hivyo midahalo hiyo itasaidia wanafunzi, kuzijua athari zake na kuepuka.

“Athari za matumizi ya dawa za kulevya ni vijana kukatiza masomo yao, kupata changamoto ya afya ya akili na kupelekea kushindwa kutimiza ndoto zao kwa kushindwa kuhitimu masomo yao,” alisema.

Aliwasisitiza washiriki wa mdahalo huo kuwa mabalozi wazuri kuhusu madhara ya matumizi ya dawa hizo shuleni na maeneo wanakoishi.

Ofisa wa taasisi hiyo, Fransisco Magoha, alitaja lengo la mdahalo huo ni kuwafundisha wanafunzi athari za kutoa rushwa katika jamii na i kuwajengea msingi mzuri wakiwa wadogo na kuwa viongozi na mabalozi wazuri katika jamii inayowazunguka.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Dodoma Mlimani, Jeniffer Mhavile, alisema midahalo hiyo ni muhimu kwa wanafunzi kwa kusaidia kuwajengea tabia ya kupinga rushwa na matumizi ya dawa za kulevya.

**Matumizi ya dawa hizo ni tatizo kubwa kwa vijana, hivyo midahalo hiyo itasaidia wanafunzi, kuzijua athari zake na kuepuka.**

# Mavunde ataja mipango kudhibiti utoroshaji madini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Madini, Anthony Mavunde, ametaja mipango ya serikali kudhibiti utoroshaji madini baada ya kuvuka lengo la ukusanyaji madini katika sekta hiyo nchini hadi kufikia Sh. bilioni 287 kwa kipindi cha miezi mitatu mwaka huu wa fedha wa 2024/25.

Akizungumza jana kwenye mjadala uliofanyika kwa njia ya mtandao kuhusu mafanikio ya serikali ya awamu ya sita katika uboreshaji wa sekta hiyo, Mavunde, alisema kwa robo ya kwanza ya Mwaka huu wa fedha wa 2024/25 kuanzia Julai-Septemba, makusanyo hayo yamevuka lengo kwa asilimia 106 kutoka Sh. bilioni 247 hadi kufikia Sh.bilioni 287.

“Tunaimarisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato na kudhibiti utoroshaji wa madini ili nchi inufaike na mapato yatokanayo na kodi, tozo na ushuru. Uanzishwaji wa masoko na vituo vya ununuzi wa madini umechangia kuleta ongezeko kubwa la mapato,” alisema.

Alisema mafanikio hayo yanatokana na mabadiliko ya sheria za madini iliyoanzisha vituo hivyo na kwamba kwa mwaka 2015/16 fedha iliyokusanywa kwenye maduhuli ya serikali Sh. bilioni 161 ziliingizwa mfuko mkuu wa serikali.

Alisema baada ya kuanzishwa kwa masoko ya madini na kudhibiti utoroshaji wa rasilimali hizo, kwa mwaka uliopita wa fedha wa 2023/24, sekta hiyo imeingiza zaidi ya Sh.bilioni 753 na kwa mwaka huu wa fedha za 2024/25, inatarajiwa kukusanya Sh.trilioni moja.

Kuhusu kuchangia pato la taifa, Mavunde, alisema mwaka 2021/22 sekta hiyo ilichangia kwa asilimia 7.2 na 2023/24 imekua na kuchangia zaidi ya asilimia tisa.

“Ili sekta iendelee kukua tumepanga kuhakikisha tunafanya utafiti wa kina wa kupima nchi nzima ili kubaini viashiria vya madini na kwenda kwenye mazoezi mengine ikiwamo kujua kiwango cha madini kilichoko,” alisema.

Alisema kwa sasa eneo ambalo limefanyiwa utafiti wa kina ni asilimia 16 na sekta hiyo kuendelea kuwa na mchango mkubwa nchini.

Waziri huyo, alisema mwaka 2022/23, sekta hiyo imeongoza kwa upatikanaji wa fedha za kigeni kwa asilimia 56 kwa kuuza bidhaa za madini nje ya nchi zenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 3.5.

Vilevile, alisema kwa mwaka huo sekta hiyo ilichangia kwa asilimia 15 ya mapato yote ya kodi ya ndani sawa na Sh.trilioni 2.1.

“Sekta ya Madini katika mwaka huo wa fedha ilichangia zaidi ya Sh. bilioni 648 kuingiza kwenye mfuko mkuu wa serikali kama maduhuli na Sh.Trilioni 1.7 zilizunguka katika mzunguko wa masoko yetu 43 na vituo vya ununuzi 102,” alisema.

Alisema mafanikio hayo yanatokana na eneo lililofanyiwa utafiti la asilimia 16, hali ambayo kwa sasa imeisukuma wizara hiyo kuja na mikakati zaidi ikiwamo dira ya mwaka 2030 ya madini ni maisha na utajiri.

“Lengo ni kuhakiki ifikapo mwaka 2030 tuwe tumefanya utafiti eneo kubwa kwa asilimia 50 ya eneo letu la Tanzania, kwa hiyo huo ni mkakati wetu wa kwanza mkubwa wa kufanya utafiti wa kina ili kulifikia eneo kubwa zaidi la nchi yetu,” alisema.

Mavunde, alisema wananchi wamehamasishana na kushiriki kwenye sekta hiyo ikiwamo kwenye upatikanaji wa ajira za moja kwa moja, utoaji huduma na uuzaji bidhaa migodini.

“Ilikuwa ni nadra sana vijana wa Kitanzania kuongoza kampuni za madini nchini na ni sehemu ya mkakati wetu wa kuhakikisha kunakuwa na ushiriki wa Watanzania,” alisema.




Mkunga Mkuu wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa Mwananyamala, Florence Uledi, akipokea msaada wa vifaa tiba vya uzazi vyenye thamani ya Sh. milioni 19 kutoka kwa Mkurugenzi wa Wateja Binafsi wa Benki ya Stanbic Tanzania, Omari Mtiga (kushoto), kwa ajili ya wodi ya wazazi katika hospitali hiyo, Dar es Salaam, mwishoni mwa wiki. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wazazi, serikali watakiwa kushirikiana kutatua vikwazo

**Na Peter Mkwavila,** CHEMBA

WAZAZI na walezi wa Kijiji cha Mondo wilayani hapa Mkoa wa wametakiwa kushirikiana na serikali kutatua vikwazo vilivyoko sekta ya elimu ili watoto wao wafanye vizuri kwenye masomo yao.

Mkuu wa Idara ya Mipango ya Mazingira wa Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini, Prof. Fadhil Mgumia, alitoa rai hiyo mwishoni mwa wiki iliyopita kwenye Mahafali ya Kidato cha Nne Shule ya Sekondari Mondo baada ya kupokea risala ya wanafunzi wakiomba kujengewa uzio wa shule hiyo ili kuondokana na mwingiliano wa watu na mifugo.

Mgumia, alisema ili kuondokana na tatizo hilo ni muhimu wazazi na walezi kushirikiana na serikali kutatua na kuweka utulivu wa watoto wao kusoma.

“Pamoja na serikali na wadau wa maendeleo ya elimu kuwa na wajibu mkubwa wa kuhakikisha na wao wachangia na kutatua changamoto zinazotokea kwenye shule, niwaombe wazazi na walezi msichukie bali mtoe ushirikiano wa kuzitatua kero hizo ili watoto wetu waweze kusoma kwa usalama zaidi,” alisema.

Awali akisoma risala hiyo, mwanafunzi Maria Zeno, alisema kumekuwapo na mwingiliano wa watu na mifugo hali na kusababisha kukosa utulivu na kuomba kujengewa uzio.

Mkuu wa shule hiyo, Alwino Luwungo, alisema mwingiliano wa mifugo kwenye eneo la shule hiyo unachangia uharibifu wa mazingira kutokana na ukataji miti iliyopandwa ili kutunza mazingira.

“Tulipanda miti 3,750 kwenye eneo hili, lakini kumekuwa na uharibifu kutokana na mifugo kupitishwa na kusababisha hasara,” alisema.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Nchemba, Said Sambala, aliahidi kushirikiana na wadau wa maendeleo ya elimu kutatua kero hiyo.





# H/shauri yaamriwa kufungua shule

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, ameiamuru Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kufungua Shule Shikizi ya Soweto iliyoko Kata ya Santilia ili kuwaondolea adha watoto na wazazi wao kutembea umbali mrefu hadi shule mama kupata elimu.

Homera alitoa amri hiyo juzi wakati akijibu ombi la wakazi wa kata hiyo kwa serikali kuwarejesha watoto shule shikizi ya Soweto baada ya kufungwa kwa kukosa vigezo vya usajili, hivyo kuwalazimu kuhamishia watoto wao shule za jirani zilizoko vijiji vingine.

**Shule hiyo haikusajiliwa kwa sababu ya kukosa vigezo na kuwashauri wananchi hao kuendelea kujenga miundombinu mingine muhimu ili isajiliwe.**

Alisema shule hiyo inatakiwa ifunguliwe na wanafunzi waendelee kusoma huku halmashauri hiyo ikiendelea na taratibu za kuisajili na wazazi kujenga miundombinu inayohitajika.

"Wazazi wamejitahidi kujenga majengo, walimu hawapo, lakini watoto wanatakiwa wasome halafu kuna watu wanazungumza mambo ya vigezo, sasa tukichukua hatua mnaanza kutuona wabaya, naagiza shule ifunguliwe watoto waendelee kusoma," alisisitiza Homera baada ya kupokea malamiko ya wakazi hao wakati akiwa katika ziara ya kukagua miradi ya maendeleo kwenye kata hiyo.

Alisema lengo la serikali kuanzisha mfumo wa shule shikizi ni kuwasaidia watoto wadogo ambao hawawezi kuifikia kirahisi, hivyo haitakiwi kuwekewa masharti magumu.

Mmoja wa wakazi hao, Ndawila Sheyo, alisema shule hiyo ilijengwa kwa lengo la kuwasaidia watoto wadogo ambao walikuwa hawana uwezo wa kwenda kusoma kwenye shule mama.

Sheyo, alisema kwa sasa wazazi wanalazimika kuwasindikiza watoto wao kwenye shule mama kila siku na kwenda kuwachukua na kukwamisha maendeleo.

"Kwa sasa ile shule imefungwa na watoto wamekosa pa kusomea tumelazimika kuwarejesha kwenye shule mama mbali sana kutoka hapa kijijini kwetu, tunaomba irejeshwe ili watoto waendelee kusoma," alisema.

Juma Oman, alisema wazazi ndio waliokuwa wanamlipa mwalimu aliyekuwa anafundisha watoto wao na wakifika darasa la tatu walikuwa wanapelekwa shule mama kuendelea na masomo.

Alisema waliambiwa kuwa shule hiyo haina vigezo vya kusajiliwa, hivyo inastahili kufungwa jambo ambalo limeanza kuwarudisha nyuma wazazi walionyesha mwamko wa kuwapeleka watoto wao shule.

Alisema wakati shule hiyo inafungwa wanafunzi waliokuwa wanasoma walikuwa 200 na madarasa yaliyopo ni matatu ambayo yalikuwa yanatosheleza mahitaji ya idadi ya wanafunzi.

Mwakilishi wa Ofisa Elimu Awali na Msingi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Mwalimu Daniel Mwala, alisema ili shule isajiliwe inatakiwa kuwa na angalau madarasa sita na matundu sita ya vyoo.

Alisema shule hiyo haikusajiliwa kwa sababu ya kukosa vigezo na kuwashauri wananchi hao kuendelea kujenga miundombinu mingine muhimu ili isajiliwe.





Vijana wakiswaga punda kuwapeleka malishoni jijini Mbeya jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Kilio kusitishwa mikopo ya mbolea, pembejeo

**Na Nebart Msokwa,** TUKUYU

WIZARA ya Kilimo imeombwa kurejeshea mfumo wa kukopesha mbolea na pembejeo nyingine za kilimo wakulima wa chai wa Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya ili kuongeza uzalishaji wa zao hilo na kukuza kipato.

Wakulima hao walitoa ombi hilo mwishoni mwa wiki iliyopita wakati wakizungumza na Nipashe wakidai kilimo cha zao hilo kimeanza kushuka wilayani humo kutokana na kukosa pembejeo.

Walisema awali walikuwa wanakopeshwa pembejeo hizo na kulipa wakati wa mauzo ya zao hilo, lakini mfumo huo uliondolewa na kutakiwa kununua pembejeo hizo kwa fedha taslimu.

Mmoja wa wakulima hao, Tusajigwa Mwakatobe, alisema miaka ya nyuma walikuwa wakikopeshwa pembejeo hizo na kukatwa wakati wa mauzo na wengi wao kuhamasika kuingia kwenye kilimo hicho.

"Tunaiomba Wizara ya Kilimo iturudishie ule mfumo wa zamani, iwe inatukopesha pembejeo na kutukata wakati wa mauzo, huu utaratibu wa sasa ni mgumu kwa sababu tunatakiwa tuuze chai ndio tununue mbolea wakati mwingine tunashindwa kuendana na msimu wa kilimo," alisema Tusajigwa.

Samwel Mwapagata, alisema miaka ya nyuma pia walikuwa wanapatiwa vifaa vya kuchumia zao hilo, kwa sasa hawapatiwi hali ambayo inasababisha kushindwa kuhudumia vizuri mashamba yao.

Alisema kwa sasa kilimo cha zao hilo kimeanza kuzorota kutokana na baadhi ya wakulima wasio na uwezo kuanza kukimbilia mazao mengine, yakiwamo maparachichi na ndizi.

Alisema chai ni miongoni mwa mazao ya biashara miaka ya nyuma yaliipa Wilaya ya Rungwe sifa, lakini kwa sasa linafifia kutokana na wakulima kunyimwa mikopo ya pembejeo.

Mratibu wa Kitengo cha Ugani wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Richard Mlelwa, alithibitisha utaratibu wa wakulima wa zao hilo kukopeshwa pembejeo kuondolewa na kwamba hawajapata pembejeo hizo kwa misimu miwili mfululizo.

Mlelwa, alisema kutokana na hali hiyo, wamelazimika kuanza kutoa elimu kwa wakulima namna ya kujitegemea kupata pembejeo hizo na wengi wameelewa na kuendelea kununua na kuhudumia mashamba na mazao yao.

Alisema wanaendelea na juhudi kuhakikisha chai inaendelea kustawi na kuwa moja ya mazao yanayoiingizia halmashauri mapato na kukuza uchumi wa wakulima na wananchi.

# Wananchi watakiwa kupima afya

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAKAZI mkoani hapa wametakiwa kujenga utamaduni wa kuchunguza afya zao ili kuepukana na vifo vya ghafla.

Rai hiyo ilitolewa jana na Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka kwenye uzinduzi wa kliniki ya kibingwa inayoendeshwa na serikali kwa kushirikiana na ubalozi wa China nchini katika viwanja vya stendi ya zamani mjini hapa.

Mtaka, alisema ni vema wakazi hao wakajenga utamaduni huo ili kujua hali za afya zao na kupata matibabu kwa wakati sahihi.

"Hapa tupo na madaktari bingwa, madaktari bobezi na vifaa, kwa hiyo kama una mgonjwa nyumbani ni vizuri mtumie hii fursa," alisema na kuongeza kuwa: "Huduma hii ni bure hakuna bima, hakuna gharama ni miguu yako tu, njoo ufanyiwe vipimo kwa sababu madawa yapo pale ambapo kuna rufani utapata rufani."

Mganga Mkuu wa Mkoa huo, Dk. Juma Mfanga, alisema ubalozi huo umeleta matibabu ya kibingwa bure ikiwamo ya magonjwa moyo na njia ya mkojo.

Balozi wa China nchini, Chen Mingjian, alisema uhusiano wa kihistoria kati ya Tanzania na nchi yake unafanya nchi hizo kushirikiana katika miradi ya maendeleo kama ya sekta ya afya kwa kuleta timu ya madaktari wa bingwa 27 kutoa huduma za kibingwa kwa wananchi.



# Wananchi watakiwa kulinda utalii

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Utalii na Mambo ya Kale, Mudrik Ramadhani Soraga, amesema sekta ya utalii ni nguzo kuu ya uchumi na kuwataka wananchi kulinda na kukuza uchumi visiwani hapa.

Soraga alitoa kauli hiyo jana wakati akizinduwa Maonesho ya Utalii wa Madili visiwani hapa.

Alisema kila mwananchi ana wajibu wa kuhakikisha analinda na kudumisha utalii wa Zanzibar kwa kuwa una manufaa kiuchumi na kuheshimu misingi ya dini na jamii.

Alisema utalii wa halali ni ule unaozingatia maadili ya dini, ustaarabu na ustawi wa jamii, hivyo kuna kila sababu ya wananchi kuunga mkono kwa sasa ili kuendelea kukuza uchumi wa Zanzibar.

Waziri huyo, alisema kuanzishwa kwa utamaduni unaoheshimu na kufuata taratibu zinazokubalika kiimani ni sehemu kubwa ya jamii ya visiwa vya Zanzibar.

"Hii ni fursa kubwa ya kutanua soko letu la utalii na kufikia wageni wengi zaidi hususan kutoka nchi za Kiislamu," alisema Soraga.

Alisema soko la utalii limekuwa likikabiliwa na changamoto mbalimbali, ikiwamo kushuka kwa kiwango cha wageni wakati wa matukio yasiyotarajiwa kama vile janga la COVID-19.

Alisema juhudi za kuimarisha utalii wa halali, zinaweza kuvutia watalii wapya ambao wanaamini na kuthamini safari zao kufanyika kwa kuzingatia maadili na imani zao.

Hata hivyo, Waziri huyo, alisema kwa upande wa Zanzibar idadi ya wageni inaongezeka siku hadi siku ukilinganishwa na wakati wa janga hilo. Alisema utalii huo unaweka misingi ya biashara na huduma zinazokubalika kidini, kuhimiza utunzaji wa mazingira, heshima kwa jamii ya wenyeji na kukuza utamaduni wa amani na utangamano.

" Zanzibar sio tu kuvutia watalii wengi zaidi, bali pia kujijenga kama kisiwa kinachofuata maadili mema na kuheshimu imani ya kila mtu," alisema Soraga.

Alisema Serikali ya Zanzibar inatambua nafasi kubwa ya sekta hiyo kuongeza ajira kwa vijana, kuimarisha uchumi wa familia, na maendeleo nchi.

"Ndiyo maana tunaendelea kuweka sera nzuri zinazolenga kuboresha sekta hii muhimu, pamoja na kukuza aina hii ya utalii wa halali unaoendana na malengo yetu ya kuendeleza uchumi wa buluu," alisema.

Soraga, alisema utalii huo umepata umaarufu katika nchi mbalimbali duniani ikiwamo Malaysia, Indonesia, Umoja wa Falme za Uarabu (UAE) na Uturuki.

"Nchi hizi zimeweza kuvutia idadi kubwa ya watalii kutoka mataifa ya kiislamu na yasiyo ya kiislamu wakiwa na uhakika wa kupata huduma zinazozingatia viwango," alisema Soraga.




Mkuu wa Idara ya KCB Sahl Banking, Amour Muro, akipokea tuzo ya kutambua juhudi za Benki ya KCB Tanzania katika kuimarisha ushirikiano wa kijamii, kutoka kwa Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, katika Kongamano la 'Light Upon Light,'jijini Zanzibar mwishoni mwa wiki. **PICHA: KCB**

# Vifo madereva vijana bodaboda kuteka kongamano maafa Z'bar

**Na Mwandishi Wetu**

AJALI za barabarani zitakuwa ajenda maalum katika kongamano la kuadhimisha Siku ya Maafa Duniani mwaka huu litakalofanyika visiwani hapa leo kutokana na kuua idadi kubwa ya vijana madereva wa bodaboda visiwani hapa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kamisheni ya kukabiliana na maafa Zanzibar, Makame Khatib Makame, alisema maadhimisho hayo kwa mwaka huu yatajikita zaidi kujenga muhimili kwa kizazi kijacho ili kuwawezesha vijana kukabiliana na majanga.

Makame, alisema kutokana na kuingiliana na matukio mengine ya kitaifa, ikiwamo Kumbukizi ya Kifo cha Mwalimu Julius Nyerere, Zanzibar juzi, siku hiyo imesogezwa hadi leo.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake jana kuhusu siku hiyo inayoadhimishwa Oktoba 13 kila mwaka, Makame, alisema kongamano hilo limepangwa kufanyika leo (Oktoba 16) katika Kampasi ya Utalii Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) Maruhubi, Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Mudrik Ramadhan Soraga, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi.

**Kamisheni hiyo imeandaa mada tatu zitakazojadiliwa katika kongamano hilo, ikiwamo umuhimu wa vijana kupunguza ajali za barabarani'.**

Mkurugenzi huyo, alisema kwa mwaka huu, Umoja wa Mataifa (UN) umetoa kauli mbiu ya maadhimisho hayo isemayo; 'Kujenga uhimili kwa kizazi kijacho katika kukabiliana na maafa.

Alifafanua kuwa kauli mbiu hiyo, imelenga kuwaelimisha vijana umuhimu wa kunusuru dunia na wao na majanga hasa yanayoweza kuzuilika.

Alisema kamisheni hiyo imeandaa mada tatu zitakazojadiliwa katika kongamano hilo, ikiwamo umuhimu wa vijana kupunguza ajali za barabarani'.

Nyingine ni 'hali halisi ya majanga na maafa Zanzibar na namna ya kuyakabili na umuhimu wa vijana kukabiliana na majanga ya moto.

Alisema licha ya serikali kuruhusu huduma ya usafiri wa bodaboda kibiashara ili kuwasaidia vijana kujiingizia kipato na kumudu maisha, wengi wao wanazitumia vibaya na kusababisha ajali kwa uzembe, mihemko rika, mwendo kasi na upakiaji hatarishi wa abiria.

Alisema takwimu zinaonesha kuwa ajali 1,72 za barabarani zilizotokea mwaka 2022 kwa vyombo vya moto na kusababisha vifo vijana hao 115 wa kiume wenye umri mdogo ambao wangekuwa nguvu kazi ya taifa kwa siku za baadaye.

Akizungumza hatua zinazochukuliwa, Makame, alisema kamisheni kwa kushirikiana na Kikosi cha Usalama Barabarani cha Jeshi la Polisi, wametoa elimu kwa waendesha bodaboda katika wilaya sita za Unguja ya ubaya wa ajali na gharama zake kwa familia na serikali.

Mbali na kongamano hilo, alisema kutakuwa na matukio mengine, ikiwemo kutoa elimu juu ya matumizi sahihi ya miundombinu, vifaa vya uokozi wa ajali za moto, baharini na matetemeko ya ardhi.

Mkurugenzi Idara ya Maendeleo ya Vijana, Shaib Ibrahim Mohammed, alisema kauli mbiu hiyo imekuja wakati mwafaka ikizingatiwa miongoni mwa changamoto nyingi za majanga hasa ajali za barabarani zinawahusu vijana.

Mohammed, alisema serikali iliruhusu usafiri wa bajaj na bodaboda kibiashara kwa vijana kwa kutoa vyombo hivyo, lakini baadhi yao wanageuza neema hiyo kwa kupuuza sheria za barabarani, kusababisha ajali, vifo, majeruhi na ulemavu, gharama za matibabu na kupandikizwa viungo vya bandia.

Alisema hali hiyo inatokana na vijana hao kukosa elimu ya uendeshaji salama wa vyombo hivyo wawapo barabarani.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**FOMU MIRATHI – 2**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya TEMEKE**
**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**
**Shauri la Mirathi Na. 1650/2024**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU RAMADHANI MUSSA LODI**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOLETWA NA ADAM R. LODI**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 5 mwezi 11 mwaka 2024 saa 2:00 asubuhi kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.
Imetokewa leo tarehe 10 mwezi 10 mwaka 2024.

HAKIMU

## KUPOTEA KWA CHETI



**SILLA MICHAEL MSULA** anatangaza kupotea kwa cheti kidato cha nne chenye index namba S2703/0036 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia Kilolo Secondary School mwaka 2013. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/MBE/KYE/19440/2024.**

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**LOYCE CHRISTOPHER EDWARD** anatangaza kupotea kwa Result Slip yenye index namba S.0332/0875 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **MOROGORO SECONDARY SCHOOL** mwaka **2024**. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/TEM/213655/2024.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU DODOMA**
**SHAURI LA RUFAA YA ARDHI NA.18956 YA 2024**
**MARTHA JUMA MTOGO........................MUOMBA RUFAA**
**DHIDI YA**
**1. FRANK BANDAGAMA YOHANA.........) WAJIBU RUFAA**
**2. ALBERT MSHANAGA.............) WAJIBU RUFAA**

**KWA: 1.FRANK BANDAGAMA YOHANA)**
**2. ALBERT MSHANAGA)**
**POPOTE PALE WALIPO**
**YAH: TAARIFA YA KUTAJWA KWA SHAURI LA RUFAA YA ARDHI NA.18956 YA 2024 MAHAKAMA KUU YA TANZANIA DODOMA**

**UNAFAHAMISHWA KWAMBA;** Shauri tajwa hapo juu litatajwa Mahakama Kuu ya Tanzania Dodoma mbele ya **MHE.E.E.KAKOLAKI,JAJI** wa Mahakama Kuu ya Tanzania Dodoma,saa tatu (3:00) asubuhi siku ya Jumatano tarehe 16/10/2024.
HIVYO:Unatakiwa ufike wewe mwenyewe au Wakili wako siku hiyo iliyotajwa bila kukosa
**NA ENDAPO:**Hutafika wewe au Wakili wako siku hiyo uliyotajwa inatosha kumaanisha kwamba shauri hili litashughulikiwa na Mahakama kama itakavyoamua pasipo wewe au Wakili wako kuwepo.
**IMETOLEWA :** Kwa mkono wangu na Mhuri wa Mahakama leo hii tarehe 11/9/2024.

..................................................
**NAIBU MSAJILI**
**DODOMA**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Hosian John Mwambiipile** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya toyota land cruiser yenye jina la Bulyhulu Gold Mine Ltd yenye usajili namba T 800 BVD. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA **PHQ/SHI/KAH/9609/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Hosian John Mwambiipile** **a**natangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya toyota land cruiser yenye jina la Bulyhulu Gold Mine Ltd yenye usajili namba T 780 BHT. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA **PHQ/SHI/KAH/9605/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

Ndugu **HAMISI ABDALLAH HUSSEINI** anatangaza kupotea kadi za pikipiki aina za Huoniao zenye namba zifuatazo:
**MC 541 CBZ chassis Na. G7EPCJL07JA014436**
**MC 542 CBZ chassis Na. G7EPCJL03JA014465**
**MC 950 BWA chassis Na. G7EPCJL07HA005195**
Kwa yeyote atakayeziona anaombwa atoe taarifa kituo cha Polisi kilicho karibu.
Amefika Polisi na amepewa Loss Report.
Taarifa Polisi: **PHQ/TAN/TAN/7168/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

Ndugu **HAMISI ABDALLAH HUSSEINI** anatangaza kupotea kadi za pikipiki aina za Huoniao zenye namba zifuatazo:
**MC 953 BWA chassis Na. G7EPC00HA005202**
**MC 951 BWA chassis Na. G7EPCJL06HA005186**
**MC 730 BGZ chassis Na. LJPCJL04BA404773**
Kwa yeyote atakayeziona anaombwa atoe taarifa kituo cha Polisi kilicho karibu.
Amefika Polisi na amepewa Loss Report.
Taarifa Polisi: **PHQ/TAN/TAN/7168/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

Ndugu **HAMISI ABDALLAH HUSSEINI** anatangaza kupotea kadi za pikipiki aina ya Huoniao yenye Namba
**MC 543 CBZ chassis Na. G7EPCJL02JA014473.**
**Na Fekon yenye Namba**
**MC 761 CAF chassis Na. LDAPAJ0B7JGB01412**
Kwa yeyote atakayeziona anaombwa atoe taarifa kituo cha Polisi kilicho karibu.
Amefika Polisi na amepewa Loss Report.
Taarifa Polisi: **PHQ/TAN/TAN/7168/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GEOFFREY GENNAR MWAIJANDE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T.836 BYC. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo karibu.
Taarifa ya polisi: **PHQ/SHI/KIS/9771/2024.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO MJINI**
**ILIYOPO MOROGORO**
**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**
**SHAURI LA MADAI/TALAKA NAMBA 28....2024**
**MDAI/MUOMBAJI LILIAN KOKUGONZA HENERICO**
**MDAIWA CLEONCE CLEOPHACE TABALO**

**Kwa: CLEONCE CLEOPHACE TABALO**
**Wa DAR ES SALAAM**
**OMBI LA MDAI/MUOMBAJI/MSIMAMIZI**
**MATUNZO YA WATOTO NA MGAWANYO WA MALI**
**MADAI YA TALAKA 28/2024**

Unatakiwa kuhudhuria hapa mahakamani katika shauri tajwa hapo juu bila ya kukosa . Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 18 mwezi 10 mwaka 2024 saa 8:30 asubuhi /alasiri
Angalia kama hukuhudhuria/hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu.
Mahakama ikithibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini, hili itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/ mmeshindwa
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hi leo tarehe 9 mwezi 10...2024

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**ABAS SAIDI OMARI** anatangaza kupotea kwa kadi ya bajaji yenye namba za usajili MC 735 DAJ – BOXER yenye Chassis namba MD2B15BX9MWD91520. Engine namba JVXWMD50532. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/209898/2024.**

**IN THE DISTRICT COURT OF MASWA**
**AT MASWA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO:25406 OF 2024**
**In the matter of Estate of the late HATUNGIMANA MABEREKERA MELCHIOR of UWANJA WA NDEGE,MASWA,SIMIYU**
**AND**
**In the matter of an application for Letters of administration by AURELIA MELCHIOR HATUNGIMANA,SARAH SAMSON KUNJI AND FILBERT NYAMUGENDA MELCHIOR.**

**GENERAL CITATION**
**{RULE 75 OF PROBATE RULES GN 369 OF 1963)**
ALL PERSONS claiming to have any interest in the state of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of the letters of administration is made to the above named petitioners.
Objections to the grant should field on or before the .....Day of .......2024.
Dated at Maswa this 08th Day of October 2024.

................................ ......................................
1st PETITIONER 2nd PETITIONER 3rd PETITIONER
Presented for filling this 10th day of October 2024

......................................
**RESIDENT MAGISTRATE**
**DRAWN AND FIELD BY:**
**PETITIONERS**
**P.O BOX 170,**
**MASWA DISTRICT**

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701**

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Piga Simu 0677020701**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Mahakama haiwezi kuzuia seneti kujadili kuondolewa Gachagua

**NAIROBI, Kenya**

WAKATI Bunge la Seneti likitarajia leo kujadili hoja za kumwondoa madarakani Naibu Rais Rigathi Gachagua, spika wa bunge hilo, Amason Kingi amesema amri za mahakama haziwezi kuzuia seneti kufanya shughuli zake.

Kauli ya spika huyo inakuja wakati Gachagua akisubiri matokeo ya kesi aliyowasilisha katika Mahakama Kuu ya Nairobi akitaka kuamriwa kusitisha kesi ya kumshtaki katika bunge la seneti.

Kutokana na msimamo huo wa Kingi, ilielezwa kuwa hatua ya Naibu wa Rais Gachagua kuzuia Bunge la Seneti kujadili hoja iliyopendekezwa ya kuondolewa kwake madarakani imepata pigo kubwa.

Alipokuwa akitoa uamuzi kuhusu suala kama hilo lililoibuliwa na Gavana wa Kericho Eric Mutai, Spika Kingi alithibitisha kwamba hakuna amri ya mahakama inayoweza kusimamisha kesi mbele ya Seneti.

"Suala la athari ya amri zozote za mahakama zinazoamuru seneti isifanye biashara yoyote limetatuliwa vyema. Katika suala hili, azimio ni sawa bila kujali msimamo uliotolewa na Bunge la Kaunti.

"Iwe ulikuwapo au laa, amri ya mahakama katika suala hili haijalishi hakuna kinachogeuzwa kuwa matokeo ni yale yale, ambayo ni kwamba Bunge haliwezi kuzuiwa kutekeleza majukumu yake ya kikatiba kwa amri ya mahakama," alisema Kingi.

Maagizo hayo ya Kingi yanaashiria kuwa uamuzi ambao Jaji wa Mahakama ya Juu Chacha Mwita, hautakuwa na athari yoyote katika kesi ya kuondolewa mashitaka dhidi ya Gachagua.

Wakati huo huo, Jaji Mkuu Martha Koome aliteua majaji watatu kwa ajili ya kusikiliza na kuamua ombi lililowasilishwa na Gachagua kupinga kuondolewa kwake mashtaka.

Koome aliwateua Majaji Eric Ogola, Anthony Mrima, na Frida Mugambi kusikiliza ombi lililowasilishwa na naibu rais anayekabiliwa na mzozo.

Katika agizo lake alilotoa katika Kitengo cha Kikatiba na Haki za Kibinadamu cha Mahakama Kuu jijini Nairobi chini ya Ombi Na. E522 la 2024, Koome alifuata maagizo yaliyotolewa na Jaji Lawrence Mugambi.

Ilielezwa kuwa Jaji Ogola ataongoza benchi iliyoteuliwa na Jaji Mkuu, na kwamba hatua za Koome zinakuja wakati hatima ya kuondolewa kwa Gachagua inatazamiwa kujadiliwa na kuamuliwa mbele ya kikao cha seneti leo.

*KTN*



Naibu Rais Rigathi Gachagua (kushoto) na Spika wa Seneti, Amason Kingi. **PICHA: MTANDAO**

# Ripoti yaibua mapya kwenye magereza Rwanda

**KIGALI, Rwanda**

SHIRIKA la Kimataifa la Haki za Binadamu (HRW) limesema vitendo vya mateso katika magereza mawili na kituo kimoja nchini Rwanda ni masuala ya kawaida kufanyika kwa wafungwa.

Kwa mujibu wa ripoti iliyochapishwa na HRW jana, ukiukaji mkubwa wa haki za binadamu, ikiwa ni pamoja na mateso, ni jambo la kawaida katika vituo vingi wanakozuiliwa watu nchini Rwanda.

Aidha, ilielezwa kuwa Aprili mwaka jana, Innocent Kayumba, aliyekuwa Mkurugenzi wa Magereza ya Rubavu na Nyarugenge, alihukumiwa kifungo cha miaka 15 jela kwa kosa la kushambulia na kumuua mfungwa katika Gereza la Rubavu mwaka 2019.

Shirika hilo lilisema limebaini hayo kwa ushahidi wa watu kadhaa waliofariki baada ya kufanyiwa mateso wakiwa wamezuiliwa gerezani.

Ilieleza kuwa ilizungumza na wafungwa kadhaa wa zamani kutoka kwenye gereza la Gacinya, kituo kisicho rasmi wanakozuiliwa watu kilicho mjini Kigali. Na kwamba ni kituo cha kwanza ambako watuhumiwa wanafikishwa baada ya kukamatwa, ikielezwa kuwa wafungwa wanalazimishwa kukiri uhalifu.

"Watu kuuawa kwa dhihaka, kupigwa na kuteswa hutumiwa na wasimamizi wa kituo kuwalazimisha kukiri makosa," ilisema sehemu ya ripoti hiyo.

Iliongeza kuwa wafungwa wa zamani wanadai kufungiwa ndani ya vyumba vidogo vyenye ukubwa wa takriban mita moja kwa mbili, sehemu ambazo, kulingana nao, zinafanana na majeneza.

Januari 2020, mwanasiasa wa upinzani Venant Abayisenga alisimulia dhuluma iliyotendwa katika kituo hicho na kudai kwamba watu waliuawa katika eneo hilo. Na kwamba mwanamume huyo alitoweka miezi mitano baadaye katika mazingira ya kutatanisha.

Ripoti hiyo pia inaandika kesi za unyanyasaji katika gereza la Nyarugenge. Ikieleza kuwa wafungwa wametoa ushahidi wao katika kesi mbalimbali kuwa waliwekwa kwa nguvu kwenye kontena lililokuwa na maji ambako walipigwa na askari magereza na wafungwa walioamrishwa kwa amri ya maofisa wa kituo hicho.

Ripoti ilibainisha kuwa mateso mengine yaliyofanywa katika gereza hilo ni pamoja na watu kunyimwa usingizi kwa kuwekwa eneo kunakopigwa muziki mwepesi na wa sauti kubwa ambao unasikika muda wote.

Hata hivyo, ripoti hiyo ilieleza kuwa katika gereza la Rubavu, wafungwa wa zamani waliripoti kupigwa mara kwa mara na Innocent Kayumba, mkurugenzi wa gereza wakati huo, kitendo ambacho kilisababisha, kulingana na shuhuda kadhaa, vifo vya wafungwa 11, na kwamba shirika hilo limehifadhi majina ya waathiriwa.

Katika ripoti hiyo, HRW inalaani „makosa makubwa sio tu ndani ya huduma za urekebishaji za Rwanda, lakini pia ndani ya mfumo wa mahakama na taasisi ya kitaifa ya ulinzi wa haki za binadamu".

Shirika hilo pia linatoa wito kwa serikali ya Rwanda kukomesha vitendo vyote vya utesaji na unyanyasaji unaofanywa kwa wafungwa.

*RFI*

## ICC kuchunguza madai ya uhalifu DRC

**KINSHASA, DRC**

MWENDESHA Mashtaka Mkuu wa Mahakama ya Uhalifu ya Kimataifa (ICC) Karim Khan, amesema anaanzisha upya uchunguzi nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) unaolenga madai ya uhalifu unaofanywa katika eneo lenye migogoro la Kivu Kaskazini tangu mwaka 2022.

Katika taarifa iliyotolewa jana na Khan alisema ghasia za hivi karibuni jimboni Kivu Kaskazini zinahusishwa na matukio ya vurugu na uhasama ambayo yamekumba eneo hilo tangu katikati mwa mwaka 2002.

Alisema kutokana na hilo, tuhuma za hivi karibuni zaidi zinaangukia kwenye uchunguzi unaoendelea, akieleza kuwa uchunguzi wa Kivu Kaskazini hautakuwa wa upendeleo.

Khan alisema uchunguzi wake huko Kivu Kaskazini hautahusisha vyama ama wanachama wa makundi maalumu lakini badala yake, ofisi yake itachunguza kiujumla, kwa njia huru, na bila upendeleo kwa wahusika wote wanaodaiwa kufanya uhalifu ndani ya mamlaka ya mahakama hiyo.

Uamuzi huo pia unafuatia rufani ya pili kutoka kwa serikali ya Kongo Mei 2023, ambayo iliomba uchunguzi katika kile ambacho nchi hiyo iliutaja kuwa uporaji wa kimfumo wa rasilimali zake asili mashariki mwa DRC kutoka kwa Jeshi la Ulinzi la Rwanda (RDF) na kundi la waasi la M23.

Aidha, ilielezwa kuwa awali mahakama hiyo ya ICC iliwatia hatiani waasi watatu kwa uhalifu katika mkoa wa Ituri, kaskazini mwa Kongo ikiwa ni pamoja na mbabe maarufu wa vita Bosco Ntaganda, anayejulikana kama 'The Terminator' ambaye alipatikana na hatia ya uhalifu ikiwa ni pamoja na mauaji, ubakaji na utumwa wa ngono.

*DW*

**Alisema kutokana na hilo, tuhuma za hivi karibuni zaidi zinaangukia kwenye uchunguzi unaoendelea, akieleza kuwa uchunguzi wa Kivu Kaskazini hautakuwa wa upendeleo.**

HABARI MICHEZO

# KOCHA SIMBA QUEENS ALIA NA UMALIZIAJI

**Na Adam Fungamwango**

LICHA ya ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Fountain Gate Princess kwenye mchezo uliochezwa juzi kwenye uwanja wa KMC Complex, Mwenge, Dar es Salaam, Kocha Mkuu wa Simba Queens, Yussif Basigi, amesema kikosi chake kina tatizo la umaliziaji, kwani licha ya kutengeneza nafasi nyingi lakini wanashindwa kuzitumia.

Akizungumza baada ya mchezo huo wa Ligi Kuu ya Wanawake, Kocha huyo ambaye ni mechi yake ya pili kuisimamia timu hiyo, akichukua nafasi ya Juma Mgunda aliyemaliza mkataba wake, alisema kama timu yake itapata mshambuliaji mzuri zaidi dirisha dogo sawa, na kama itakuwa ni kuwanoa hawa hawa waliopo, basi hilo litakuwa jukumu lake.

„Tunahitaji mmaliziaji mzuri, huwezi kufika langoni na kupata nafasi kila muda, hivyo unapopata nafasi unatakiwa kuitumia vizuri, tunatengeneza sana nafasi, sasa kama tukipata wamaliziaji wazuri mbele ya safari, au tuwatengeneze na kuwanoa hawa hawa, tutafunga mabao mengi sana,“ alisema kocha huyo raia wa Ghana aliyekuwa akiifundisha klabu ya Hasaacas Ladies ya nchini humo.

Akiizungumzia mechi hiyo, alisema kipindi cha kwanza walitawala lakini walipoteza nafasi nyingi, kipindi cha pili wapinzani wao walipopata bao moja mpira ukabadilika ukawa na presha zaidi, hadi pale walipopata bao la tatu.

„Kipindi cha kwanza tulitawala mpira, ila tulipoteza nafasi nyingi, hicho nataka kukifanyia kazi, ukifunga mabao machache unampa mpinzani wako kujituma kurudisha, angalia tumefunga mawili, walipopata bao moja walitushambulia sana ili kurudisha, kwa bahati tukapata bao la tatu lililomaliza mchezo,“ alisema.

Yalikuwa ni mabao ya Elizabeth Wambui, Precious Christoper na Jentrix Shikangwa yaliyoipa ushindi Simba Queen na kufikisha pointi sita, baada ya mchezo wa kwanza kuifunga Mlandizi Queens mabao 3-0, mechi iliyochezwa TFF Centre, Kigamboni, Dar es Salaam.

Wakati Simba Queens ikipata ushindi mara mbili mfululizo, Yanga Princess ililazimishwa suluhu dhidi ya Alliance Girls, Uwanja wa Nyamagana, Mwanza.

Ni sare ya pili kwenye Ligi Kuu, baada ya mchezo wa kwanza kufungana bao 1-1 dhidi ya Bunda Queens, mechi iliyochezwa Uwanja wa Karume, Musoma, Mara.




Katibu Tawala Wilaya ya Kinondoni, Warda Abdallah, akikabidhi kombe la mshindi wa jumla kwa Nahodha wa Timu ya Maendeleo, Isaac Acton, baada ya kuibuka mabingwa kwenye bonanza la kuadhimisha ya miaka 40 ya SGA. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kikapu taifa kuanza kutimua vumbi

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya Kimataifa ya mpira wa kikapu yanatarajiwa kuanza kutimua vumbi leo mpaka Oktoba 20 kwenye viwanja vya Filbert Bayi, Kibaha mkoani Pwani.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa Shirikisho la Mpira wa Kikapu Tanzania (TBF), Mary Arthur, alisema mashindano hayo yatashirikisha klabu mbalimbali kutoka nje ya nchi ambapo kwa upande wa Tanzania itawakilishwa na timu ya JKT.

"Maandalizi yanaendelea vizuri kuelekea kwenye mashindano hayo ambayo yatakuwa na mvuto kutokana na nchi zitakazoshiriki, alisema Arthur.

Alisema baadhi ya timu zitaanza kuwasili jijini Dar es Salaam wiki hii kwa ajili ya kushiriki mashindano hayo yatakayohusisha timu kutoka Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi na wenyeji Tanzania.

Alisema mashindano hayo yatasaidia kuimarisha viwango vya wachezaji na kuwataka Watanzania wajitokeze kwa wingi kuangalia vipaji vitakavyokuwa vikionyeshwa na wachezaji hao.

Alisema kwa sasa mchezo huo unazidi kushika kasi tofauti na ulivyokuwa miaka iliyopita kwa vijana wengi kuonekana kuupenda na kuuelewa.

"Tunashukuru kwa sasa mchezo huu unazidi kukua na kushika kasi tofauti na ulivyokuwa miaka iliyopita kwani watu wengi wanaupenda mchezo wa kikapu,“ alisema.

# Zimamoto 'yafufuka' Zanzibar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya Zimamoto SC imefanikiwa kupata ushindi wake wa pili katika michezo sita aliyocheza mpaka sasa kwenye Ligi Kuu ya Zanzibar.

Ushindi huo wa pili wameupata baada ya juzi kuwafunga wanajeshi wa Kipanga FC mabao 2-1 katika mwendelezo wa Ligi Kuu ya Zanzibar, mchezo huo uliochezwa kwenye uwanja wa nje wa Amaan 'Annex B'.

Akizungumza na gazeti hili Kocha Mkuu wa Zimamoto SC, Mohamed Hilali alisema licha ya kupata ushindi huo amekiri kuwa mchezo ulikuwa mgumu.

Alisema kikubwa walichofanikiwa katika ushindi huo ni wachezaji wake kutokata tamaa hata walipotanguliwa kufungwa bao moja na wapinzani wao katika kipindi cha kwanza.

Alisema walicheza kwa matumaini na malengo ili kuhakikisha hawapotezi mchezo ambao muhimu kwa kila mzunguko.

Aidha, aliweka wazi kuwa kikosi chake hakijapata mrithi wa nafasi ya ushambuliaji baada ya kumuuza mshambuliaji wao, Ibrahim Hilika aliyetimkia Tanzania bara.

Alisema kutopata watu sahihi katika nafasi hiyo ya ushambuliaji ndio inawafanya kushindwa kupata mabao licha ya kutengeneza nafasi nyingi.

"Tumeshinda lakini bado hatupo vizuri katika safu ya ushambuliaji, tunakosa magoli mengi ya wazi, tumekuwa tukipoteza nafasi nyingi ambazo tunazitengeneza kwa bidii," alisema.

Timu ya Zimamoto SC imepanda mpaka nafasi ya tisa ikitokea nafasi ya 11 baada ya kufikisha pointi nane wakati wapinzani wao Kipanga FC wakibakia nafasi ya 12 na pointi zao nne.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MAN KUMPIGA BEI MAGUIRE
KLABU ya Manchester United inajiandaa kumuuza mlinzi wa England, Harry Maguire mwenye umri wa miaka 31 katika dirisha dogo la Januari. ***(Star)***

### MUSTAKABILI WA HAALAND MAN
MSHAMBULIAJI wa Norway, Erling Haaland mwenye umri wa miaka 24 ameamua kuhusu mustakabali wake mbali na Manchester City, lakini hatajiunga na Paris St-Germain. ***(El Nacional)***

### EDERSON ATAFUTIWA MRITHI
MANCHESTER City ina nia ya kumsajili mlinda mlango wa Ureno, Diogo Costa mwenye umri wa miaka 25 kutoka Porto kama mbadala wa muda mrefu wa Mbrazil Ederson mwenye umri wa miaka 31. ***(Football Insider)***

### FERNANDEZ AWINDWA LALIGA
REAL Madrid na Barcelona zinavutiwa na Mhispania mwenye umri wa miaka 21 wa Benfica na beki wa zamani wa Manchester United, Alvaro Fernandez Carreras. ***(O Jogo)***

### CHELSEA YAMTAKA GITTENS
CHELSEA, Tottenham Hotspur na Liverpool zimetuma maskauti kumtazama winga wa Borussia Dortmund na timu ya taifa ya England kwa vijana chini ya umri wa miaka 21, Jamie Gittens katika wiki za hivi karibuni. ***(Bild)***

### MAINOO NA MKATABA MPYA
KIUNGO wa kati wa England, Kobbie Mainoo mwenye umri wa miaka 19, anasalia kwenye mjadala kuhusu mkataba mpya na Manchester United lakini hakuna makubaliano yaliyofikiwa.***(Fabrizio Romano)***

### OMORODION NA REAL MADRID
MSHAMBULIAJI wa Porto na Hispania, Samu Omorodion mwenye umri wa miaka 20 amesema Mungu ndiye aliyemfanya kushindwa kuhama kutoka Atletico Madrid kwenda Chelsea msimu wa majira ya joto uliopita. ***(Metro)***


### BAYERN HAINA MPANGO NA BECKER
KLABU ya Bayern Munich haivutiwi na mlinda lango wa Liverpool na Brazil, Alisson Becker mwenye umri wa miaka 32, licha ya mashaka kuhusu mustakabali wa Manuel Neuer katika klabu hiyo. ***(ESPN)***

### JAMES NI BARCA AU BENFICA
MLINZI wa kulia wa Chelsea na England, Reece James mwenye umri wa miaka 24, anatazama kupitia wawakilishi wake uwezekano wa kujiunga na Barcelona au Benfica. ***(Football Transfers)***

### KERKEZ ATAKIWA ARSENAL
ARSENAL inapanga kuwasilisha dau la kumnunua beki wa kushoto wa Bournemouth na Hungary, Milos Kerkez mwenye umri wa miaka 20, na winga Antoine Semenyo mwenye umri wa miaka 24, mchezaji wa kimataifa wa Ghana. ***(CaughtOffside)***

### HOWE KUBAKI NA NEWCASTLE
KOCHA wa Newcastle United, Eddie Howe mwenye umri wa miaka 46, hana mpango wa kuondoka katika klabu hiyo licha ya kuwa miongoni mwa watu walioorodheshwa kwa ajili ya kazi ya kuinoa England. ***(Telegraph)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# DEST AMVAA KOCHA WA ZAMANI, XAVI

●●●Beki huyo amelalamika kocha wa zamani hakumtendea haki mpaka kufikia...

**ASMTERDAM, Uholanzi**

BEKI Sergiño Dest amesema kocha wa zamani wa Barcelona, Xavi Hernández hakumtendea haki baada ya kuondoka katika klabu hiyo na kwenda PSV Eindhoven kwa mkataba wa kudumu mapema mwaka huu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 alijiunga na Barca kutoka Ajax mwaka 2020 wakati Ronald Koeman bado alikuwa kocha, lakini alipata nafasi ngumu katika kikosi cha kwanza baada ya Xavi kuteuliwa kuwa kocha Mkuu mwaka mmoja baadaye.

Beki huyo wa pembeni wa Marekani alisema Xavi hakumpa nafasi za kutosha kujidhihirisha, alizuia uchezaji wake na kutotimiza ahadi alizompa.

"Ningesema majuto, kwa sababu jinsi yalivyoisha haikutegemea, lakini sijisikii nilikuwa na nafasi muhimu nikiwa na Xavi," alisema Dest akiiambia Diario Sport kuhusu miaka yake minne kama mchezaji wa Barca.

"Nilihisi kama lazima nicheze kwa mipaka kwamba siwezi kuwa mimi mwenyewe. Nataka kujiunga na mashambulizi ambayo ndiyo nguvu yangu kubwa, lakini aliniomba nisiende mbele.

"Sidhani pia alikuwa mkweli kwangu. Tulifanya mazungumzo kadhaa ambapo aliniambia jambo moja lakini baadaye nilikuwa na mashaka kama aliniambia ukweli.

"Katika majira ya joto ya 2023, kabla ya kwenda likizo, aliniambia: ,Ninakutegemea, usisome magazeti.' Na mara niliporudi, aliniambia: ,Lazima uende' akimaanisha niondoke kwenye kikosi hicho'.

Dest alitumia msimu wa 2022-23 kwa mkopo katika klabu ya AC Milan ya Italia na mwaka jana huko PSV kabla ya kujiunga tena na klabu hiyo ya Uholanzi msimu uliopita wa majira ya joto, lakini hapo awali alikuwa ameanza maisha kwa matumaini huko Barca.Chini ya Koeman, alikuwa mchezaji wa kikosi kilichoshinda Copa del Rey mwaka wa 2021, lakini aliishia kupoteza imani chini ya Xavi.

"Nilikuwa nikisafiri kwa ndege nilipofika," aliongeza. Mambo yalikwenda vizuri kwa mtu binafsi. Lakini mwishowe, nilikuwa mpya hapa, wachezaji wenzangu hawakunijua.

"Mtindo wangu ni kujihatarisha na mpira lakini niliombwa kucheza tofauti. Hilo lilinifanya nipoteze imani katika maamuzi yangu, una shaka kuwa wewe mwenyewe au kubadilisha mtindo wako. Mashaka hayo yanaharibu uchezaji wako."

Dest kwa sasa yuko nje ya uwanja kutokana na jeraha la goti na anatarajiwa kurejea uwanjani mwaka mpya, lakini ana mwelekeo wa kurejea kwenye ligi moja kubwa barani Ulaya siku zijazo.

# Mendy aidai Man City bilioni 390

**MANCHESTER, England**

BEKI wa zamani wa Manchester City, Benjamin Mendy amesema alikopeshwa fedha na wachezaji wenzake, Raheem Sterling, Bernardo Silva na Riyad Mahrez wakati klabu hiyo ilipoacha kumlipa mshahara baada ya kushtakiwa kwa ubakaji na unyanyasaji wa kingono, aliiambia mahakama ya ajira.

Beki huyo wa Ufaransa anadai mshahara wa pauni milioni 11.5 (zaidi ya shilingi bilioni 390) ambao hakulipwa tangu aliposhtakiwa Agosti 2021 na kusimamishwa bila malipo na Man City.

Mendy mwenye umri wa miaka 30, alifutiwa mashtaka mwaka 2023.

Klabu hiyo iliendelea kumlipa Mendy baada ya kukamatwa kwa mara ya kwanza Novemba 2020, lakini walidai kuwa hawakulazimika kufanya hivyo baada ya kushtakiwa kwa kuwa masharti yake ya dhamana, moja wapo yalimzuia kwenda karibu na uwanja wa klabu au uwanja wa mazoezi na shirikisho la soka lilimaanisha kuwa kwa kusimamishwa kwake asingeweza kutekeleza majukumu yake ya kimkataba.

Nyaraka za mahakama zilisema Mendy „aliishiwa fedha haraka sana" na ilimbidi kuuza jumba lake la kifahari la Cheshire ili kulipia ada za kisheria za kesi, malipo ya matumizi na matunzo ya watoto baada ya kuzuiliwa kwa mshahara wake.

"Raheem Sterling, Bernardo Silva na Riyad Mahrez wote walinikopesha fedha ili kunisaidia kujaribu kulipa ada yangu ya kesi na kusaidia familia yangu," alisema Mendy katika taarifa yake ya ushahidi.

Novemba 2022, Mendy alituma ujumbe wa Whatsapp kwa Omar Berrada, ambaye alikuwa ofisa mkuu wa uendeshaji wa soka wa Man City kuanzia Septemba 2020 hadi Julai 2024, kuuliza ni lini atapokea mishahara yake isiyolipwa lakini hakujibiwa.

# Nigeria yasusia mechi dhidi ya Libya

**TRIPOLI, Libya**

NIGERIA imejiondoa katika mechi yao ya kufuzu kwa Kombe la Mataifa ya Afrika dhidi ya Libya kwa mujibu wa nahodha wao William Troost-Ekong na Shirikisho la Soka la Nigeria (NFF), ikipinga kutelekezwa uwanja wa ndege kwa saa 16.

Super Eagles walipaswa kucheza na wenyeji Libya katika jiji la Benghazi ambako walitarajia kutinga kinyang'anyiro cha kufuzu kwa fainali hizo zitakazofanyika Morocco mwishoni mwa mwaka ujao.

Lakini baada ya kukwama kwa zaidi ya saa 16 kwenye uwanja wa ndege ulio umbali wa kilomita 250 kutoka walikokusudia, wachezaji wa Nigeria walisema hawatatimiza ratiba na NFF ilitoa taarifa.

"Wajumbe wa Nigeria kwenye mechi ya Jumanne ya kufuzu AFCON 2025 dhidi ya Libya bado walisalia kwenye Uwanja wa Ndege wa Al Abraq saa 12 baada ya kutua Libya," ilisema taarifa hiyo.

„Ndege iliyokodishwa ya ValueJet, kwa njia ya ajabu na ya hatari, ilielekezwa kwenye uwanja mdogo wa ndege mbali na Benghazi wakati rubani alipokuwa akikamilisha safari yake kuelekea Uwanja wa Ndege wa Benghazi.

"Wachezaji na maofisa waliochoka wamesalia bila furaha kwani mwenyeji Shirikisho la Soka la Libya lilishindwa kutuma timu yoyote ya mapokezi au hata magari kuwachukua wajumbe kutoka uwanja wa ndege hadi hoteli yao, ambayo inasemekana kuwa umbali wa saa 3 huko Benghazi.

„Wachezaji wameamua kutocheza mechi tena kwani maofisa wa NFF wanapanga mipango ya kurudisha timu nyumbani."

Troost-Ekong alisema kwenye X: "Kama nahodha, pamoja na timu, tumeamua kwamba hatutacheza mchezo huu. Inaonekana ndege yetu inaongezewa mafuta tunapozungumza na tunapaswa kuondoka kwenda Nigeria hivi karibuni."

CAF ilisema katika taarifa yake kuwa wamewasiliana na mashirikisho ya soka ya nchi zote mbili na kwamba "suala hilo limepelekwa kwenye Bodi ya Nidhamu ya CAF kwa uchunguzi na hatua stahiki zitachukuliwa kwa wale waliokiuka Sheria na Kanuni za CAF."

Shirikisho la Soka la Libya limesema tukio hilo halikuwa la makusudi na limeitaka Nigeria kuwa na uelewa.

„Tuna heshima kubwa kwa wenzetu wa Nigeria na tunataka kuwahakikishia kwamba kukengeushwa kwa safari yao ya ndege haikuwa kwa makusudi," ilisema, na kuongeza kuwa usumbufu unaweza kutokea kutokana na itifaki za kawaida za trafiki ya anga, ukaguzi wa usalama au changamoto zingine za vifaa.

„Tunakataa kwa uthabiti madai yoyote yanayopendekeza mchezo mchafu au hujuma katika hali hii. Tunatumaini kwamba kutoelewana huku kunaweza kutatuliwa kwa maelewano na nia njema."



# NEYMAR TAYARI KUREJEA DIMBANI

**RIYADH, Saudi Arabia**

MSHAMBULIAJI wa Brazil Neymar ameimarika haraka katika kupona goti lake na anaweza kurejea uwanjani Oktoba 21, vyanzo viliiambia ESPN Brasil.

Nyota huyo wa Al Hilal amekuwa nje ya uwanja kwa mwaka mmoja tangu apate majeraha katika goti lake la kushoto alipokuwa kwenye majukumu ya kimataifa na Brazil.

Neymar mwenye umri wa miaka 32, alirejea kufanya mazoezi na Al Hilal Septemba 29.

Watu wanaofuatilia kwa karibu maendeleo ya Neymar wanaamini kuwa mchezaji huyo anaweza kurejea kucheza kwa wakati kwa ajili ya mchezo wa Al Hilal wa Ligi ya Mabingwa Asia Uwanja wa Al Ain Oktoba 21.

Kocha wa Al Hilal, Jorge Jesus ndiye atakuwa na sauti ya mwisho kuhusu Neymar atarejea lini kwenye mechi za ushindani.

Hata hivyo, atahitaji kwanza idhini ya daktari wa timu ya Brazil Rodrigo Lasmar, ambaye alimfanyia upasuaji Neymar.

Lasmar anatarajiwa kusafiri hadi Saudi Arabia siku zijazo kutathmini utimamu wa mchezaji huyo.

Neymar, ambaye ni mfungaji bora wa muda wote wa Brazil, alijiunga na timu ya Saudi Pro League Agosti 2023 kutoka Paris Saint-Germain lakini alicheza mechi tano tu kabla ya kuumia.

Shirikisho la Soka la Brazil linafuatilia kwa karibu hali hiyo na linatumaini kuwa Neymar atapatikana kwa wakati kwa mechi za kuwania kufuzu kwa Kombe la Dunia Novemba dhidi ya Venezuela na Uruguay.

HABARI MICHEZO

# BACCA, RUPIA, VINARA MABAO YA VICHWA LIGI KUU

**Na Mwandishi Wetu**

BEKI wa kati wa Yanga, Ibrahim Hamad ,Bacca', mshambuliaji wa Singida Black Stars, Elvis Rupia na John Makwata wa Coastal Union, wanaongoza kwa kufunga mabao ya vichwa mpaka sasa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Hadi kufikia kwenye michezo ya raundi ya saba, wachezaji hao wamepachika mabao mawili kwa kutumia kichwa, kiungo ambacho kinaruhusiwa kutumika kwenye mchezo wa mpira wa miguu.

Kwa mujibu wa takwimu za dawati la michezo la Nipashe, jumla ya mabao 18 yamefungwa kwa vichwa mpaka sasa, huku vinara wa kufunga mengi wakiwa ni wachezaji hao.

Rekodi zinaonyesha kuwa Bacca alifunga bao lake la kwanza, Septemba 25, Uwanja wa Sokoine Mbeya, akiiwezesha Yanga kushinda bao 1-0 dhidi ya KenGold, akarudia tena kufunga kwa kichwa Oktoba 3, Uwanja wa Azam Complex, katika mchezo ambao timu yake ilishinda mabao 4-0 dhidi ya Pamba Jiji FC.

Rupia, raia wa Kenya, alipachika bao kwa kichwa, Agosti 17, mwaka huu, Uwanja wa Sokoine, Mbeya akiiongoza timu yake kushinda mabao 3-1 dhidi ya KenGold, akarudia tena Septemba 12, Uwanja wa Liti, Singida, wakati timu yake iliposhinda mabao 2-1 dhidi ya KMC.

Mbali na hao, straika mwingine ni Makwata wa Coastal Union, ambaye anakamilisha wachezaji watatu waliopachika mabao mengi kwa kichwa kwenye Ligi Kuu.

Alifunga bao la kufutia machozi, Septemba 21, mwaka huu, Coastal ikipoteza mabao 2-1 dhidi ya JKT Tanzania na Septemba 28, ilipoifunga Pamba Jiji mabao 2-0.

Wachezaji waliofunga bao moja moja na kukamilisha idadi ya mabao 18 ya vichwa mpaka sasa ni Mohamed Damaro wa Singida Black Stars, Che Fondoh Malone, Valentino Mashaka na Edwin Balua, wote wa Simba, Peter Lwasa na Obrey Chirwa, wote wa Kagera Sugar, Andy Bikoko wa Tabora United, Wilson Nangu wa JKT Tanzania, Jacob Massawe wa Namungo, Abalkassim Khamis wa Fountain Gate, na Lusajo Mwaikenda wa Azam FC.



Mchezaji wa Timu ya Soka ya International All Stars (IAS) wenye umri chini ya miaka 11, Michael Salota (kulia), akijaribu kuruka juu ya wachezaji wa Timu ya Soka ya Dar Thunders (DTFC) kwenye mchezo wa ufunguzi wa mashindano ya vijana ya ,Dar Youth Cup 2024' yanayofanyika Uwanja wa TPDC Mikocheni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Geita Gold yajitutumua Championship

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Geita Gold imepata ushindi wake wa pili kwenye Ligi ya Championship, ikiwa ni azma yake ya kutaka kurejea Ligi Kuu Tanzania Bara, ilipoifunga Kiluvya FC bao 1-0 katika mchezo uliochezwa juzi kwenye Uwanja wa Jamhuri Morogoro.

Baada ya ushindi huo, Geita Gold iliyoshuka daraja msimu uliopita, imepanda hadi nafasi ya tano katika msimamo wa ligi hiyo, ambayo inasaka timu tatu zitakazopanda Ligi Kuu msimu ujao.

Bao pekee la washindi lilifungwa na winga wa zamani wa Kagera Sugar, Yanga na Simba, Yusuph Mhilu, aliyeunganisha kwa kichwa mpira uliorushwa na beki wa pembeni, Adeyum Salehe.

Geita Gold imecheza mechi nne mpaka sasa ikishinda mbili na sare mbili, ikikusanya pointi nane mpaka.

Kwa kipigo hicho, Kiluvya FC inaendelea kushika mkia, ikiwa haina pointi wala bao kwenye ligi hiyo mpaka sasa ikicheza michezo minne.

Kabla ya mechi hiyo majira saa nane mchana kwenye uwanja huo huo, kulikuwa na mchezo kati ya Transit Camp, dhidi ya Polisi Tanzania ulioisha kwa suluhu.

Matokeo hayo yanaifanya Polisi Tanzania kushika nafasi ya 11 ikiwa na pointi nne, huku Transit Camp ikiwa nafasi ya 15 na pointi yake moja.

Mechi nyingine ilikuwa kwenye Uwanja wa Ilulu, Lindi, Bigman ikipata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Cosmopolitan.

Shaaban Kinawa alianza kuiandikia Bigman bao la kwanza, Sadick Said aliisawazishia Cosmopolitan kipindi cha pili, kabla ya beki wa zamani wa Stand United, Ihefu, KMC na Yanga, Ally Ally, kufunga bao la pili.

Bigman imefikisha pointi saba ikiwa nafasi ya nane, huku Cosmo ikiwa nafasi ya 14 na pointi moja.

## Stars yanyong'onyesha mashabiki nyumbani

INATOKA UK. 24

viongozi wa Stars tu, bali hata wachezaji kwani hawakuonekana tena kufanya juhudi kama mwanzo.

Wachezaji wa DR Congo walipasiana mpira winga ya kulia bila kusumbuliwa na baadaye mpira ulimkuta Fiston Mayele aliyeingia kipindi cha pili kuchukua nafasi ya Simon Banza, akampenyezea tena Elia ambaye alionekana ni hatari anapokuwa kwenye eneo mpinzani, aliwahadaa mabeki wa Stars na kupiga shuti la kiufundi lililokwama wavuni kuiandikia Congo bao la pili na kuipeleka timu yake kwenye fainali hizo za Morocco.

Matokeo hayo yanaifanya DR Congo kushinda mechi zake zote nne na kufikisha pointi 12 ikiongoza kundi.

Stars sasa itakuwa na kazi ya kugombea nafasi moja iliyobaki na Ethiopia pamoja na Guinea.

Dakika za mwanzo tu za mchezo, Stars ilifanya shambulizi kali baada ya krosi ya Clement Mzize iliyokuwa ikienda kutua kwenye vichwa vya wachezaji, Feisal Salum na nahodha Mbwana Samatta, lakini kipa Dimitry Bertaud anayecheza katika klabu ya Montpellier ya Ufaransa, aliruka juu ya kuugusa mpira huo na kuokoa hatari golini kwao.

Samatta alikosa bao la wazi dakika ya 12, alipobaki na golikipa Bertaud, baada ya kupenyezewa pasi murua na Mudathir Yahaya, lakini shuti lake lilipaa juu ya lango huku kocha Suleiman Hemed ,Morocco', akiwa tayari amesimama akijiandaa kushangilia.

Dakia sita baadaye, DR Congo ilijibu shambulio hilo pale Eddo Kayembe, alipopiga shuti la mbali la kushtukiza lakini mpira ukaishia mikononi mwa Ally Salim.

Kibu alikaribia kufunga bao dakika ya 38 baada ya kuunganisha kwa kichwa mpira wa krosi kutoka kwa Samatta, lakini ukatoka sentimeta chache na kugonga nyavu za nje.

Kipindi cha kwanza, Stars ilionekana kufanya mashambulizi mengi huku kwa kiasi kikubwa wapinzani wao walikaa nyuma ya mpira na kushambulia kwa kushtukiza.

Kipindi cha pili Congo walibadilika kiuchezaji kwa kuanza kulishambulia lango la Stars mfululizo na kuonekana kuwa hatari zaidi wakiwa na mpira.

Timu zote zilifanya mabadiliko ambapo Stars iliwatoa Lusajo Mwaikenda, Mudathir na Mzize nafasi zao zikichukuliwa na Bakari Mwamnyeto, Himid Mao na Selemani Mwalimu mabadiliko ambayo hata hivyo hayakuisaidia kuepuka kipigo hicho cha pili kwenye kundi lao.

## Michuano CHAN kuathiri ratiba ya Ligi Kuu Bara

INATOKA UK. 24

ipo na klabu zipo zinaweza kulisemea, ila kwetu sisi tutalazimika kufanya marekebisho ya ratiba kutokana na kalenda hiyo ya CAF, kupisha CHAN na mechi za kimataifa," alisema Kasongo.

# Michezo

Jumatano Oktoba 16, 2024

Nipashe

## Dest amvaa kocha wa zamani, Xavi

UKURASA 21





Mshambuliaji na Nahodha wa Taifa Stars, Mbwana Samatta (kulia), akimtoka beki wa Congo, Nathaniel Mbuku katika mchezo wa Kundi H wa kufuzu fainali za Afrika 'Afcon 2024' jana kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# STARS YANYONG'ONYESHA MASHABIKI NYUMBANI

## ●●●Yakubali kipigo kwa Congo, matumaini kufuzu Afcon 2024 yamebaki kwa...

**Na Mwandishi Wetu**

WINGA Meshack Elia anayeichezea klabu ya Young Boys ya Uswizi, jana aliifungia mabao yote mawili timu yake ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo na kuwa ya kwanza kufuzu kucheza fainali ya Mataifa ya Afrika (AFCON) kutoka Kundi H na kuiweka kwenye wakati mgumu Taifa Stars.

Stars ikicheza kwenye uwanja wa nyumbani iliwanyong'onyesha mashabiki wake kwa kukubali kipigo hicho ambacho sasa kimeiweka Tanzania njia panda katika kufuzu fainali za Afrika za mwakani zitakazofanyika nchini Morocco.

Mashabiki wengi walikuwa na matumaini ya Stars kufanya vizuri kwenye mchezo baada ya kuonyesha uwezo mkubwa kwenye mchezo wa kwanza uliochezwa Kinshasa wiki iliyopita ambao pia Stars ililala kwa bao 1-0.

Matokeo hayo yameifanya Stars kusalia na pointi zake nne baada ya kucheza michezo minne na sasa imebakisha michezo miwili dhidi ya Guinea na Ethiopia ambayo ni lazima washinde yote ili kufuzu kwa mara ya nne fainali hizo.

Kuendelea kushika nafasi ya pili kwenye kundi lake itategemea na matokeo ya mchezo wa jana usiku kati ya Ethiopia watakaocheza na Guinea kwenye mchezo wa marudiano baada ya mchezo wa kwanza Guinea kuibuka na ushindi wa mabao 4-1 na kufikisha pointi tatu, pointi moja nyuma ya Stars.

Endapo Guinea itapata ushindi kwenye mchezo huo itapanda mpaka nafasi ya pili kwa kufikisha pointi sita na kuiweka Stars kwenye wakati mgumu zaidi.

Katika mchezo wa jana ulioanza saa 10:00 jioni, Elia aliingia uwanjani kipindi cha pili kuchukua nafasi ya Mvupa Katompa na kuwashangaza Watanzania kwa mabao hayo mawili ya kipindi cha pili.

Alikuwa Masuaku Kamwela aliyeambaa na mpira kwenye winga wa kulia, alipotanguliziwa mpira na Gedeon Kalulu aliyemnyang'anya Kibu Denis mpira na kupiga krosi ambayo ilionekana kama haina madhara, lakini iliunganishwa kwa mguu wa kushoto na Elia.

Mpira huo ulidunda nchini na kumpoteza golikipa Ally Salim aliyeuangalia mpira ukijaa wavuni.

Bao hilo lilionekana kuwanyong'onyesha si mashabiki na

INAENDELEA UK. 23

# Michuano CHAN kuathiri ratiba ya Ligi Kuu Bara

**Na Adam Fungamwango**

UWEPO wa Fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wanaocheza Ligi za Ndani (CHAN), kumetajwa kuwa kutaathiri moja kwa moja ratiba ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi, Almasi Kasongo, alisema mabadiliko ya ratiba za Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF) kwenye michuano ya CHAN na Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho, moja kwa moja yataathiri ratiba hiyo, hivyo watakaa na kufanya marekebisho.

"Tunaendela kufanya marekebisho na maboresho ya ratiba baada ya Kamati ya Utendaji ya CHAN kukaa na kufanya marekebisho ya ratiba zao.

Fainali ya CHAN zimepangwa kufanyika hapa Tanzania, Kenya na Uganda kuanzia Februari Mosi mpaka 28, lakini pia kuna mechi za 'play off' za kwenda kucheza hizo fainali ambazo zitaanza Oktoba 25 hadi 27, maana yake wamekuja kuathiri ratiba yetu moja kwa moja," alisema Kasongo.

Alisema pia kutokana na hayo, ni lazima wafanye marekebisho ya ratiba ya Ligi Kuu ili kuruhusu wachezaji watumikie timu yao ya taifa.

Mbali na hilo, Kasongo pia alisema CAF imebadilisha pia ratiba za Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho ambalo kwa kawaida lilitakiwa lichezwe mwezi Oktoba, sasa linararajiwa kuanza Novemba hadi Januari hivyo kuathiri pia Kombe la Mapinduzi ambalo hufanyika Januari Mosi hadi 13 mwakani.

"Januari kuna Kombe la Mapinduzi, lakini kwenye ratiba ya CAF kutakuwa na michezo ya Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho timu za Simba na Yanga zikiwapo.

Ikumbukwe Simba na Yanga kushiriki michuano ya Kombe la Mapinduzi, lakini kipindi hicho watakuwa kwenye mechi za makundi, ingawa kwa hili sitaki sana kuelezea, kamati yenyewe

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >